# KAMA ILIVYOKUWA SIKU ZA NUHU

## Ngano na magugu

## Mavuno

## Mwisho wa nyakati

## Ushindi wa kanisa

**Paul Galligan**

**Revival Ministries Australia**

# YALIYOMO

| | Ukurasa |
|---|---|
| **Utangulizi** | **3** |
| **Katika nyumba ya Baba yangu** | **4** |
| **Watenda kazi kwa anjili ya mavuno** | **12** |
| **Ngano na magugu** | **19** |
| **Uhakika wa kunyakuliwa**<br>Sehemu ya kwanza: mafundisho ya kunyakuliwa yalitoka wapi? | **24** |
| **Uhakika wa kunyakuliwa**<br>Sehemu ya pili: kufufuliwa wafu | **29** |
| **Uhakika wa kunyakuliwa**<br>Sehemu ya tatu: Yesu atashuka kutoka mbinguni. | **33** |
| **Uhakika wa kunyakuliwa**<br>Sehemu ya nne: kumlaki Bwana hewani | **35** |
| **Kama ilivyokuwa siku za Nuhu** | **38** |
| **Injili ya ushindi** | **48** |
| **Maneno muhimu katika Mathayo 24:39- 41** | **43** |

# UTANGULIZI

## Kitabu hiki ni cha waamini waliokomaa

Tunaachilia kitabu hiki kwa onyo: mafundisho katika **kitabu hiki ni ya waamini waliokomaa.** Sio ya wakristo wachanga lakini kwa wale wamefika katika kiwango cha ukomavu na wameandalika kwa mafundisho ya Neno la Mungu, Biblia, kama ilivyoandikwa,

## Mafundisho ya kusikilika

Katika urejesho wa Yerusalemu na hekalu ya Mungu katika kitabu cha Nehemia, wakati kuta zilijengwa upya, Ezra Mwandishi alikuja na kikundi cha Walawi na akafundisha neno la Mungu kwa watu wote. Maandiko yanasema, ***"Nao wakasoma katika kitabu, katika torati ya Mungu, kwa sauti ya kusikilika; wakaeleza maana yake, hata wakayafahamu yaliyosomwa"*** **(Nehemia 8:8).**

Katika historia ya agano la kale, watu wa Mungu kupitia waalimu wao, waliendelea kuondoka katika mafundisho ya sheria ya Musa, na kuamini mafundisho yaliyokuwa hayajapatikana yaliyoletwa kwao na manabii wa uongo. Walimu wa kweli, kama Ezra na manabii waandishi, waliinuliwa na Mungu kulifundisha neno la Mungu, wakiwaita watu wairudie sheria ya Musa.

## Kuchangamoto fundisho la kunyakuliwa

Katika sehemu hizi za mafundisho tunaangalia vifungo vya maandiko ambavyo vinajulikana vyema sana lakini zimefudishwa kama elimu iliyopotoka.

Elimu hii inazungumzia matukio ya nyakati za mwisho na inaleta maoni yasio katika maandiko ya kusudi la Mungu duniani na hatima ya watakatifu katika Kristo.

Fundisho linajulikana kwa jumla kuamini katika 'kunyakuliwa' kwa watakatifu [kanisa] kutoka hapa ulimwenguni. Mafundisho haya yamebadilisha elimu ya kurudi mara ya pili kuwa kurudi mara mbili: kuja mara ya kwanza ya Yesu kutoka mbinguni kunyakua kanisa kisirisiri hapa duniani, kuiacha dunia chini ya utawala wa 'mpinga Kristo'; na sehemu ya pili ya kurudi ni Kristo kuja pamoja na watakatifu kwa hukumu.

## Uweni Waberea wazuri (Mdo 17:11)

Tunakuhimiza unaposoma kitabu hiki kuangalia kila andiko na kusoma kila kifungo kufahamu na kuelewa mafundisho halisi ambayo Roho Mtakatifu anatuletea kutoka kwa Biblia. Iweni macho kutochukua mawazo yaliofikiliwa katika maandiko, lakini soma andiko kama ilivyoandikwa, pasina kuongezea, au kupunguza kutoka kwake.

Waberea walikuwa "***waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo"***

# KATIKA NYUMBA YA BABA YANGU

## FUNDISHO KATIKA YOHANA 14:2 KATIKA MAZINGIRA YA MAANDIKO

Moja yapo ya aya ambazo zimetafsiriwa vibata katika Biblia ni **Yn 14: 2**: ***"Nyumbani kwa Baba yangu kuna makao mengi; kama sivyo, ningeliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali"***.

- Swali la kwanza: nyumba ya Baba ni nini?
- Swali la pili: makao ni nini?
- Swali la tatu: Yesu alikuwa akienda wapi?
- Swali la nne: Yesu alikuja tena?
- Swali la tano: Yesu anatupokea kwa jinsi gani kwake?

### Kanuni ya muktadha

Hebu tujiburudishe na kanuni ya muktadha. Kila aya ya maandiko ni lazima kwanza ieleweke katika muktadha ya kifungo ambacho inapatikana. Kisha aya ionekane katika muktadha; kisha katika muktadha ya kitabu; kisha katika muktadha ya agano; kisha katika muktadha ya Biblia yote.

## YESU ALIKUWA AKIENDA WAPI?

### Mazungumzo

**Yohana 14** inaonekana katika mazungumzo na Petro ambayo yalianza katika **Yn 13:36**. Mazungumzo haya yalianzia katika chakula cha mwisho – Yesu na wanafunzi wake wakisherehekea chakula cha pasaka Yerusalemu. Yesu tayari alikuwa amewatawadha wanafunzi wake miguu; tayari alikuwa amemtambua msaliti wake na yuda alikuwa ameondoka kwenda kukitenda kitendo cha kutisha. Yesu alikuwa amewapatia wanafunzi amri mpya ya kupendana mmoja na mwingine. Kisha Petro akauliza, ***"Bwana, unakwenda wapi? Yesu akamjibu, Niendako huwezi kunifuata sasa; lakini utanifuata baadaye"*** **Yn 13:36.**

### Yesu alikuwa anaenda Yerusalemu kuteseka

Petro alitaka kujua Yesu alikuwa akienda wapi. Alijua kwamba Yesu alikuwa akienda mahali. Yesu alikuwa akiwaandaa wanafunzi kwa muda, akiwaambia ni lazima aende Yerusalemu ***"na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka"*** **(Mt 16:21).** Wakati Yesu aliwaambia wanafunzi ya kuwa walikuwa waende na Yesu kwa Lazaro baada yake kufa, Tomaso alisema, ***"Twendeni na sisi, ili tufe pamoja naye"*** **(Yn 11:15-16).** Wanafunzi walijua na walihusika kuwa Yesu alikuwa akienda kufia Yerusalemu. Haya ndio muktadhaYesu aliuliza, ***"unakwenda wapi?"***

### Petro angefuata baadaye

Yesu alisema kwamba Petro hangeenda naye kwa wakati huo lakini Petro angemfuata baadaye. Baada ya kufufuka, Yesu alimwambia Petro ***"Amin, amin, nakuambia, Wakati ulipokuwa kijana, ulikuwa ukijifunga mwenyewe na kwenda utakako; lakini utakapokuwa mzee, utainyosha mikono yako, na mwingine atakufunga na kukuchukua usikotaka''*** **Yn 21:18.** Yesu alikuwa akimuambia Petro ***"ni kwa mauti gani atakayomtukuza Mungu. Naye***

***akiisha kusema hayo, akamwambia, 'Nifuate'"* (aya 19).** Petro alikuwa na hatima ya kumfuata Yesu hata kifo, lakini sio wakati huo.

## Petro hakuwa tayari

Turejelee mazungumzo kama ilivyoandikwa katika **Yn 13**, ***"Petro akamwambia, Bwana, kwa nini mimi nisiweze kukufuata sasa? Mimi nitautoa uhai wangu kwa ajili yako?* (aya 37).** Petro alijua kwamba Yesu alikuwa akienda kwa mauti yake. Petro alikuwa akimshawishi Yesu kwamba alitaka kufa pamoja naye, lakini Yesu alijua vyema! ***"Yesu akajibu, je! Wewe utautoa uhai wako kwa ajili yangu? Amin, amin, nakuambia, Jogoo hatawika hata wewe utakapokuwa umenikana mara tatu"* (aya 38).**

Yesu anamtabiria Petro sio tu kwamba Petro hayuko tayari kufa naye lakini atamkana Yesu usiku huo huo.

## Yesu alikuwa akikutana na kifo

Unaweza kuona mazingira ya swali la Petro 'Bwana, unakwenda wapi?' ilikuwa ni katika mazingira ya ufahamu kwamba Yesu alikuwa akutane na mauti yake katika Yerusalemu? Tunajua vyema akiwa na ufahamu kwamba Yesu alikuwa akienda msalabani.

Alikuwa tayari amesalitiwa! Alikuwa katika chakula cha mwisho! Alianzisha meza ya Bwana usiku huo – ***"ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate"* (1Kor 11:23)!**

## Yohana 14

Kisha tunakuja kwa ile inaitwa **sura ya 14 ya Yohana,** lakini kumbuka kwamba sura na aya ziliongezwa katika Biblia baadaye na hazikuwa katika nakala za kwanza. Mgao huu wa aya unakuja katikati ya <u>**mazungumzo ya Petro na Yesu.**</u>

## Yesu anaendelea kuzungumza na Petro

Akiisha tu kutabiri Petro kumkana Yesu, kisha Yesu akasema naye, "***msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu; niaminini na mimi"* Yn 14:1.**

Yesu mara anampa Petro mwelekeo: '*Petro, utakapofika mahali hapa pakuu pa kuvunjika moyo, ukiisha tambua uliyoyatenda, chochea imani yako katika Mungu; lakini utahitaji zaidi ya imani ya kuyumba yumba katika Mungu, utahitaji kuniamini, Yesu!*' haya ni mashauri ya ajabu jinsi gani!

Ni watu wangapi husema wanamwamini Mungu lakini hawana imani inayofanya kazi katika Yesu Kristo?

## NYUMBA YA BABA NI NINI?

Kisha Yesu akasema, ***"katika nyumba ya Baba yangu"!*** Nyumba ya Baba ni nini? Ni mbinguni? Wengi wanadhania ni mbinguni, lakini maandiko yanasema nini?

### Katika <u>agano la kale</u>

Katika agano la kale, nyumba ya Mungu ilikuwa ni hekalu katika Yerusalemu, katika vitabu vya **Wafalme** na **Mambo ya nyakati,** hekalu katika Yerusalemu ilikuwa ndiyo NYUMBA ya Mungu. Hata katika kitabu cha Hagai, hekalu inaitwa "***nyumba"*** [ikitafsiriwa 'hekalu' lakini kimsingi nyumba].

#### Kulikuwa na vyumba vingi

Zaidi, nyumba ambayo Sulemani alimjengea Mungu ilikuwa ***"Nao ukuta wa nyumba akauzungushia vyumba, kushikamana na nyumba kote kote, za hekalu na za chumba cha ndani; akafanya vyumba vya mbavuni pande zote"*** **1Wafalme 6:5.** Nyumba ya Mungu katika agano la kale ilikuwa na vyumba vingi ndani yake. Vilikuwa vimetengenezwa na Sulemani ili makuhani wavitumie.

#### Yeremia alikutana katika moja wapo wa hivyo vyumba

Katika **Yeremia 35**, Mungu alimwambia Yeremia awalete wana wa Rekabi ***"ukawalete nyumbani kwa BWANA, katika chumba kimoja"*** **aya 2.** Yeremia akawaleta ***"ndani ya chumba cha wana wa Hanani, mwana wa Igdalia, mtu wa Mungu, kilichokuwa karibu na chumba cha wakuu"*** **aya 4.** Wakuu walikuwa pia na chumba ambacho wangekutana na watu, wale na wanyue, na pengine wapumzike, nyumba ya Mungu ilikuwa na makao mengi!

#### Nyumba ya Mungu ni nyumba ya maombi

Katika **Isaya 56,** nyumba ya Mungu inaitwa ***"nyumba ya sala kwa mataifa yote" aya 7.*** Wageni ambao ***"waliandamana na BWANA ili wamhudumu, …. hao nao hata … na kuwafurahisha katika nyumba yangu"*** **(aya 6-7).** Hata katika Agano la Kale, nyumba ya Mungu ilijengwa ili watu wote waweze kusongea kwa Mungu ili <u>wapate mahali pa kudumu Naye duniani.</u>

### Nyumba ya Mungu ni nini katika <u>Agano Jipya?</u>

Wakati Yesu aliingia hekaluni katika **Mt 21:12-16**, aliitakasa kutoka biashara zote, ***"akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua"*** **aya 12.** Akatangaza, ***"imeandikwa, <u>Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala</u>"*** **aya 13.** Yesu alitambua hekalu kama nyumba ya Mungu, hata kuiita 'nyumba yangu', kama alivyokuwa Mungu katika mwili! Baada ya Yesu kuitakasa hekalu, "***vipofu na viwete wakamwendea mle hekaluni, akawaponya"*** **Mt 21:14.** Kuna uponyaji katika nyumba ya Mungu.

#### Yeye aliyeijenga nyumba

**Ebr 3:1-6** inazungumza habari za Yesu mtume na ujenzi wa nyumba ya Mungu. Katika **aya 3**, Yesu anatajwa kama ***"yule aitengenezaye nyumba".*** Katika **aya 6,** nyumba ni yake Kristo, ***"bali Kristo, kama Mwana, juu ya nyumba ya Mungu; ambaye nyumba yake ni sisi …".*** Sio tu kwamba Yesu ndiye mwenye nyumba lakini, ***<u>sisi, watu wake, ndio nyumba!</u>*** Hii ni ya kupendeza na ya ajabu namna gani?

#### Nyumba ni kanisa

Paulo alimwandikia Timotheo ili apate ***"kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli"*** **1Tim 3:15**. Katika agano jipya, kanisa ni nyumba ya Mungu, na Yesu kama mtume wa Mungu, aliyetumwa kutoka mbinguni, analijenga kanisa, nyumba ya Mungu! Yesu alisema kwa Petro, ***"na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda"*** **Mt 16:18.** Petro alikuwa ndiye jiwe la kwanza la msingi ambaye Yesu alitumia kuanza kulijenga kanisa, nyumba ya Mungu.

Nyumba ya Mungu ambayo ni kanisa la Mungu aishiye ni pahali ambapo **ukweli** unapatikana: ukweli kuhusu Mungu! ***"Mungu alidhihirishwa katika mwili!"*** **1Tim 3:16**

### “*Katika nyumba ya Baba yangu!”*

Hakuna sababu ya kufikiria nyumba ya Baba iko mbinguni katika hali ya kibiblia inayozungumzia nyumba ya Mungu. Katika Biblia, nyumba ya Mungu inaongea kuhusu <u>makao ya Mungu ya kudumu hapa duniani.</u>

Mungu anakusudia kuimarisha makao yake ya kudumu duniani na watu: ***“Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao”*** **Ufu 21: 3.** Kutajwa huku katika **Ufu 21** iko katika mazingira ya Yesu Kristo kuja duniani. Anasema, ***“Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo”*** **Ufu 22:12.**

## ‘MAKAO’ NI NINI?

### Kuna *“makao mengi’*”

Vizazi vingi vya waumini wamepotoshwa kufikiri kwamba Mungu pengine anawajengea nyumba mbinguni, na sio nyumba ya kawaida, lakini nyumba kubwa! Neno la Kiyunani ni ‘mone’.

> SC# 3438 Kiyunani, *mone*: Neno hili la Kiyunani limetumika mara mbili tu katika agano jipya: Katika Yn 14:2 nyumba kubwa; mara ingine ambayo hili neno la Kiyunani linatumika katika agano jipya ni katika Yn 14:23 “Yesu akajibu, akamwambia, mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake [abode KJV]”
> Neno la Kiyunani halimaanishi Nyumba kubwa, kama nyumba ya mtu tajiri, kwa vyovyote. Kwa kifupi inamaanisha pahali pa kudumu, pa makao.

### Kwa nini neno <u>nyumba?</u>

Waamini wengi wanaota kuhusu nyumba zao mbinguni, wengine wanafikiria Yesu anawanjengea nyumba zao sasa. Wengine wanasema malaika wanashughulika wakiwanjengea nyumba zao mbinguni. Ili hali <u>Mungu anajiandaa kuja duniani kudumu na watu</u>. Mpango wa Mungu ni kuijaza dunia na utukufu wake; hajabadilika katika kusudi hilo.

### Tutakuwa kama malaika

Wakati unafikiria jinsi unaweza kuwa mbinguni, ni kwa nini ufikirie kuwa na nyumba kama za ulimwenguni? Yesu alisema tutakuwa kama malaika mbinguni. Malaika hawana nyumba kwa maana hawana mahitaji ya kawaida ili wawe na nyumba mbinguni. Wala watakatifu hawahitaji nyumba mbinguni kwa maana hawatakuwa na mahitaji ya kawaida ili wawe na nyumba mbinguni!

### Yawezekana kuwe na nyumba nyingi ndani ya nyumba moja?

Sehemu ya kwanza ya **Yn 14:2** inasoma: ***“nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi”.*** Katika lugha ya Kingereza, hii haina maana: inawezekanaje kuwe na nyumba kubwa nyingi ndani ya nyumba moja. Nyumba kwa maelezo inaweza kuwa na vyumba vingi, hata gholofa nyingi katika jengo moja, lakini nyumba haiwezi kuwa na nyumba nyingi ndani ya nyumba moja. Leo kunakuwa na majengo mengi makuu lakini hatusemi kuna nyumba nyingi katika nyumba; huwa tunasema kwamba kuna majengo mengi ambapo watu wanaishi.

### Nyumba kubwa?

Matumishi ya neno 'mansion/nyumba kubwa' sio sahihi na inapotosha, haisaidii kuyaelewa maandiko. Katika **Nehemia,** makuhani na walawi ***"wakasoma katika kitabu, katika torati ya Mungu, kwa sauti ya kusikilika; wakaeleza maana yake, hata wakayafahamu yaliyosomwa.*** **Nehe 8:8**

### Yesu anaijenga nyumba duniani

Wakati Yesu alikuja mara ya kwanza alileta ufunuo wa utukufu wa Mungu duniani ukifunuliwa ndani ya mwanadamu: ***"nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli"*** **Yn 1:14.**

Sasa Yesu analijenga kanisa lake hapa ulimwenguni, mwili wenye washiriki wengi/viungo ambao atafunua utukufu wake kwao; ***"na wote wenye mwili watauona pamoja".*** **Isaya 40:5.**

Ni ***"Kristo ndani yetu tumaini la utukufu":*** huu ni ufunuo wa ***"utajiri wa utukufu wa siri katika Mataifa"*** **(Kol 1:27).**

- Kanisa ndio nyumba ya Mungu;
- Kanisa limejengwa na washiriki/viungo vingi;
- Kanisa ni nyumba ya kiroho inayojengwa na mawe yaliyo hai **(1 Pet 2:5)**;
- Kanisa ni jengo, ***"mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni"*** **Efe 2:20**
- Kanisa **linakua** kuwa ***"hekalu takatifu katika Bwana"*** **aya 21**
- Kibinafsi, mwili wa waamini ni ***"hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu"*** **1Kor 6:19.**
- Kwa pamoja tumeitwa ***"sisi tu hekalu la Mungu aliye hai"*** **2Kor 6:19.**

***Sisi tu makao ya Mungu, kibinafsi na kwa pamoja***

## KWENDA KUANDAA MAHALI

### *"Naenda kuwaandalia mahali"*

- Yesu alikuwa akienda wapi? alikuwa akiandaa mahali kwa njia ipi kwetu?
- Mahali ni nini? Mahali ni mahali pa kudumu, kuishi, kukaa ndani.
- Tunaishi wapi? Tunadumu wapi?
- Tunadumu katika Kristo; tunazaliwa upya katika Ufalme wake; tunabatizwa katika Kristo.

Tunapompokea Yesu, tunazaliwa na Mungu (**Yn 1:13).** Tunakuja mahali ambapo Yesu anatuandalia katika nyumba ya Baba. Uhai wetu ***"umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu"*** **Kol 3:3.**

Kutoka tuzaliwe mara ya pili tunakua! Tunakua tupajaze mahali ambapo Yesu alituandalia. Hatimaye mahali hapo ni mahali pa ufunuo wa utukufu wa Mungu; ni mahali pa kuujua utukufu mkuu ***Kristo ndani Yetu, tumaini la utukufu.*** Ni mahali pa uwana mkomavu, tukiisha kukua kutoka kwa utoto katika Kristo na tukiisha kutumika kama vijana wake na waume katika injili, tunapokea mahali katika nyumba ya Baba; tunapokea urithi wa mwana na tunatembea katika uhusiano huo wa uwana na Baba.

### Kuteseka na kufa

- Yesu alikuwa akienda Gethisemane (**Yn 18:1).** Ona **Lk 22:39-46, Mk 14:32-42, Mt 26:36-46.**
- Kisha Yesu akakamatwa akapelekwa mbela ya waandishi na wazee [baraza la viongozi wa wayahudi] (**Mt 26:57-68).**
- Kisha Yesu akapatianwa kwa Pilato, liwali wa Rumi. Wakati pilato "***baada ya kumpiga Yesu mijeledi, akamtoa ili asulibiwe" (Mt 27:11-26).***
- Alikutana na Herode, mfalme wa wilaya ya Galilaya (**Lk 23: 6-12),** na akamtuma kwa Pilato.
- Akaelekezwa aende kusulibiwa (***Mt 27: 31-44),***
- Yesu alikufa msalabani (**Mt 27:45-56).**
- Yesu alizikwa katika kaburi ya Yusufu (**Mt 27:57-61).** Pilato akaweka walinzi kuilinda kaburi (**Mt 27:62-66).**

### Yesu alikuwa akienda msalabani

Yesu alikuwa akienda wapi? **Yesu alikuwa akienda msalabani,** akikusudia na akitaka. Alikuwa akienda kutuandalia mahali. Alikuwa akienda msalabani kutuwezesha kuja kwa Mungu; kutuwezesha kuishi na Mungu katika mahali anapotuweka katika nyumba yake, ambayo tumetambua ni kanisa lake duniani.

Yesu alituandalia mahali kwa kumwaga damu yake, jia pekee ambayo kwa hiyo tunaondolewa dhambi zetu. Yesu alikwenda kwa kifo kwa ajili yetu. Aliyatoa maisha yake kwa ajili yetu, kila mara akijua kwamba ana uwezo wa kuyachukua tena.

### Yesu alikwenda kuzimu

Wakati mwili wa Yesu ulikuwa kaburini, Yesu, ***"alihuishwa roho yake",*** alikuwa akiyakamilisha mambo kadha wa kadha katika himaya ya roho, katika mahali hapo kwa kawaida panaitwa 'kuzimu'. Katika **1Pet 3:18-20,** ***"aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri";*** katika **Efe 4:8-10,** ***"naye alishuka mpaka pande zilizo chini za nchi"*** **(aya 9).**

Katika **Mdo 2:24** ***"uchungu wa mauti"*** ambao Yesu aliachiliwa kutoka kwake, ni 'utungu'; ***Yesu*** alikuwa akileta viumbe vipya**.** Hii ndiyo kazi kuu ambayo alikuwa anakamilisha wakati mwili wake ulikuwa kaburini. Wengine wamefunza kwamba ibilisi na mapepo walikuwa wakimletea Yesu uchungu alipokuwa kuzimu. Hii haingewezekana kwa kuwa Yesu alikuwa Mungu katika Roho na shetani hawezi kamwe kumgusa Mungu katika Roho; angekuja tu kinyume cha Mungu akifunuliwa katika mwili.

### Yesu aliienda kwa Baba

Mariamu Magdalene alikuwa wa kwanza kumwona Yesu akiwa hai kutoka kwa wafu. Hakumtambua – ni lazima alikuwa tofauti! Wakati Yesu aliongea jina lake akatambua ni nani alikuwa akizungumza naye. Ona hadithi hii ya ajabu ikifunguka katika **Yn 20:11-16.**

Kisha Yesu akamwambia, ***"usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba Yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu"*** **Yn 20:17.** Katika asubuhi hiyo ya kufufuka huko kwa ajabu, Yesu alikuwa na jukumu moja kuu la kutekeleza, kukamilisha kazi ya ukombozi. Alikuwa akienda kwa Baba. Alikuwa akienda mbinguni kukamilisha kazi; alikuwa aichukue damu yake mbinguni na aiweke katika kiti cha rehema.

### Mbinguni hasa

**Waebrania** inatuambia kwamba Yesu, ***"aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu"*** **9:24.** Aliingia ***"wala si kwa damu ya mbuzi na dama. Bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele"*** **Ebr 9:12.** Hili lilikuwa ni jukumu la mwisho kutekelezwa kukamilisha ukombozi, kushinda mauti kikamilifu kwa kuondoa dhambi zote kabisa.

Wakati Yesu aliwatokea wanafunzi wake wakiwa wamekusanyika pamoja Yerusalemu, alikuwa tofauti kuliko wakati Mariamu alikuwa amemwona. Alisema, ***"tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo"*** **Lk 24:39.** Kisha akawauliza kitu cha kula, ***"wakampa kipande cha samaki wa kuokwa. Akakitwaa, akala mbele yao"*** **aya 42-43.**

### Yesu alikuwa na uwezo wa 'kuonekana' kutoka kwa UTUKUFU!

Yesu alikuwa kwa Baba; Yesu alikuwa ameipeleka damu yake mbinguni hasa na sasa alidhihirika katika mwili uliotukuzwa. Haya ni magumu kuelewa lakini imenakiliwa vyema kwetu.

Wanafunzi walikuwa wamekusanyika katika milango iliyofungwa ***"kwa hofu ya Wayahudi"*** na ***akaja Yesu, akasimama katikati"*** **Yn 20:19. Mdo 1:3** inatuambia Yesu ***"kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai".*** Yeye aliyekuwa amejidhihirisha kama mwana wa Adamu alikuwa sasa anajidhihirisha kama mwana wa milele wa Baba.

### YESU ALIKUJA TENA

Yesu alikuwa amewaahidi wanafunzi wake ***"nitakuja tena"*** **Yn 14:3.** Kwa sababu ya kutafsiri vibaya **Yn 14:2**, wengine hata wameamini kwamba hii inazungumzia kuja kwa Kristo mara ya pili. Hata hivyo ni lazima tusome kila aya na kila maelezo katika kila aya katika mazingira ya kitengo. Yesu anaenda msalabani kufa. Aliwaambia wanafunzi wake ya kuwa atakuja tena kwao. Anazungumzia kufufuka kwake lakini wengi wetu kama wanafunzi wa Yesu, tuna wepesi wa kufahamu.

Siku tatu baadaye Yesu **alikuja tena!** ***"ikawa jioni, siku ile ya kwanza ya juma, pale walipokuwapo wanafunzi, milango imefungwa kwa hofu ya Wayahudi; akaja Yesu, akasimama katikati, akawaambia, Amani iwe kwenu"*** **Yn 20:19.** Yesu alikuja tena kama alivyoahidi. Siku tatu baadaye wanafunzi walimwona. Baada ya hayo "***wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arubainne, na kuyanena mambo yaliyouhusu ufalme wa Mungu"*** **Mdo 1:3.**

### YESU ANATUPOKEA NAMNA GANI KWAKE?

Yesu alisema ***"nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo"*** **Yn.14:3b.** Wakati Yesu alikuja tena kwa wanafunzi wake, aliwahudumia amani – waliogopa na kutishika! Kisha akawaambia alikuwa anawatuma kwa njia ile ile ambayo Baba alikuwa amemtuma (**Yn 20:21**). Kisha ***"akawavuvia, akawaambia, pokeeni Roho mtakatifu"*** **Yn 20:22.**

Wakati Yesu alikuja tena aliwapokea wanafunzi wake kwake; akawahudumia amani, ***"Amani ya Mungu, ipitayo akili zote"*** **Flp 4:7,** na akawavuvia Roho Mtakatifu katika maisha yao. Haya hayangetendeka kabla ya msalaba.

Kwa sababu ya dhambi wanadamu hawangepokea Roho Mtakatifu wa Mungu katika maisha yao. Wangemjua Mungu tu kwa Roho akija juu yao kama upako kuwawezesha kufanya jambo fulani.

Lakini kwa sababu Yesu alikuwa msalabani kuziondoa dhambi zote, wanafunzi wangepokea amani ya Mungu isiyo ya kawaida; wangepokea Roho wa Mungu katika maisha yao.

### Je, na sisi leo?

Yesu anatupokea aje? Yesu alinipokea siku ambayo, nilipozaliwa mara ya pili. Alinipokea kwake. Kwa dakika hiyo nilipata kumjua Yesu binafsi. Sijawahi kosa kuwa nayeye tangia wakati huo. Maisha ya Kikristo ni maisha ya kukua katika mahali hapo ambapo Yesu ametuandalia msalabani; kukua katika mahali hapo ambapo Mungu ametupa katika mwili wa Kristo, Kanisa lake.

Baada ya kuzaliwa mara ya pili kwa Roho, tunabatizwa katika Kristo Yesu. Ubatizo ni utimilifu wa hicho ambacho kilianza kwa kuzaliwa upya. Kama tumebatizwa kwa jina la Yesu katika msingi wa toba, Petro anasema tutapokea karama ya Roho Mtakatifu (**Mdo 2:38**). Utimilifu wa Uungu ungedumu ndani yetu kuanzia wakati huo.

### Yesu yuko wapi leo?

Yesu alikwenda kwa Baba. Yesu alikwenda ndani ya pasia, katika himaya ya milele ya mbinguni. Kuingia himaya hiyo, ufalme huo, ni lazima tuwe tumezaliwa upya kwa Roho wa Mungu. Nikodemo alitaka kufahamu jinsi angelikuwa na Yesu. Akatambua kwamba Yesu alikuwa ametoka kwa Mungu. Alitaka kuwa na Yesu. Yesu akamwambia ya kwamba njia ya pekee ilikuwa ni kwa kuzaliwa upya. Yesu akasema, ***"Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu"*** **Yn 3:5.**

- Nyumba ya Baba ni kwa jia nyepesi, mwili wa Kristo.
- Imempendeza Mungu kutupatia mahali katika mwili (**1Kor 12:18**).
- Makusudi ya Mungu ni kwa kanisa lake liwe bibi arusi wake, mke wake.
- Mungu atakaa na watu wake, kanisa lake, duniani.

**Hii itakuwa maonyesho ya mwisho ya mapenzi ya Mungu:<br>nyumba ya Mungu ikiwa imejengwa kikamilifu, ikidhihirika kikamilifu duniani.**

# WATENDA KAZI KWA AJILI YA MAVUNO

## Omba Bwana wa mavuno

***"Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji"*** **Mt 9:35-36.** Katika ujuzi huu Yesu alisema kwa wanafunzi wake, ***"mavuno ni mengi lakini watenda kazi ni wachache, basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake"*** **aya 37-38.**

## Mavuno ni watu wa Mungu

Katika mazingira ya ujuzi wa Yesu, mavuno ni nini na ni wafanyi kazi wa aina gani wataifanya kazi ya 'kuvuna' katika mavuno haya? Yesu alikuwa akiona umati wa watu wa Israeli, watu wa Mungu, kama kondoo wasio na mchungaji. Hii inamaanisha kwamba Yesu anatarajia watu wake wakue mpaka ukomavu. Watu tayari ni wake lakini wanahitaji watenda kazi ambao ni wachungaji wa kweli – wachungaji ambao ni wa moyo wa Mungu – kuwaleta katika ukomavu.

***"Nami nitawapa ninyi wachungaji wanipendezao moyo wangu, watakaowalisha kwa maarifa na fahamu"*** **Yer 3:15.**

## Yesu aliwatuma watenda kazi

Katika jawabu ya msemo wake wa hitaji la watenda kazi, kisha Yesu alitaja na akawatuma wale thenashara waanze kufanya kazi ya huduma miongoni mwa watu wa Mungu. Yesu alichagua na akatuma mitume katika mavuno. Akawapa nguvu juu ya ***"pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina"*** **Mt 10:1.** Akawaambia ***"kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia"*** **aya 7.**

Yesu alizungumzia mavuno tena katika **Lk 10:2**, akiyanena maneno yale yale tena kwa wanafunzi wake kama alivyofanya katika **Mt 9:37-38**. Wakati huu ilikuwa ni katika mazingira ya Yesu kuwachagua wengine sabini na kuwatuma ***"wawili wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe"*** **Lk 10:1.**

Mazingira ni yale ya huduma ya Yesu kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Hawa sabini walikuwa wamtangulie Yesu kumwandalia njia kutembelea miji mingine mingi na jiji. Yesu tena analenga mavuno miongoni mwa watu wa Mungu; sio mavuno ya nafsi mpya zikija katika ufalme wa Mungu, lakini mavuno ya ukomavu na mazao ikija kutoka kwa watu wa Mungu.

## Karama za huduma zinatakiwa kuleta kanisa katika ukomavu

Makusudio wazi ya Mungu katika agano jipya ni kujenga kanisa lake. Anafanya haya kwa kupatiana **'karama kwa wanadamu'**; ***"Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu"*** **Efe 4:8-11.** Karama hizi za huduma zinapatianwa na zinatakiwa kufanya kazi ya huduma ***"kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapo ufikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa***

***Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*** **aya 12:13.**

Tambua kwamba mwinjilisti ni mmoja wa karama ambazo Yesu alipatiana katika kupaa kwake kuleta kanisa katika ukomavu. Kurushwa kwa uinjilisti wa duniani yote katika miaka iliyopita ni ya kusifiwa; lakini kanisa ambalo linaonekana kama matokeo sasa ni kama watu wa Mungu ambao Yesu alikuwa akizungumzia katika **Mt 9:35-36**. Yesu aliona uweza wa mavuno. Sio haswa nafsi mpya, lakini ni kuwaleta watu wa Mungu kila mahali kwa kuifanya kazi ya huduma. **Haya ndiyo mavuno.**

### Mimea tayari kwa mavuno

Nikiendesha kupitia kusini mwa mashariki mwa Queensland (mji ninaoishi) mapema 2010, niliona wimbi ukisimama mashambani ukiwa na afya. Ilionekana imeiva sana na nikashangaa ni kwanini hapana mtu wa kuvuna. Katika Australia, uvunaji unafanywa na machine kubwa na nafaka haiwezi kuvunwa ila kuwe na hali ya anga ikiwa kavu. Kama kiwango cha nafaka kina maji mengi, kitatoa jasho na kuoza baada ya kuvunwa. Kwa njia ingine hali ya mavuno inapaswa kuwa inafaa.

Baada ya hayo nikaota kuhusu mavuno. Baadhi ya wapendwa wangu walionekana katika ndoto. Nilikuwa na wakati mgumu kuwashawishi ndugu zangu kwamba mavuno yako tayari; ni lazima twende kazini.

**Ni wakati wa ukomavu kwa sababu ukomavu ni wakati wa mavuno.**

### Mavuno ni mwisho wa nyakati

Yesu alisema, ***"mavuno ni mwisho wa dunia; na wale wavunao ni malaika/ wajumbe"*** **Mt 13:39b.** Watu wengi wanaamini kuwa tuko katika mwisho wa nyakati kwa sababu nyingi tofauti, lakini mara nyingi watu wanaamini kwamba tuko mwisho wa nyakati kwa sababu ya ishara ambazo wanaamini kwamba ndio utimizo wa 'maandiko ya kinabii'. Watu wengi wanaonekana kuwa na mitazamo tofauti kuhusu mambo ya siku za mwisho.

Ni vyepesi na wazi kuenenda na yale ambayo Yesu alisema kuhusu mavuno. Hatuwezi kufanya zaidi kuhusu uharibifu wa kawaida na misukosuko ya kisiasa katika mataifa; hatuwezi kufahamu utedaji wa uchumi wa dunia; lakini tunaweza kuwa tayari kwa mavuno, hivyo ni, tunaweza kufanya kazi ya huduma kulileta kanisa katika ukomavu (**Efe 4:11-16**).

## MAVUNO NI KUWAHUDUMIA KONDOO WALIOPOTEA WA ISRAELI

Wakati Yesu alitaja kwanza mavuno katika **Mt 9:37-38**, ilikuwa ni katika mazingira ya kondoo waliopotea wa Israeli ambao alikuwa akitafuta na kuwahudumia (**aya 35-36**). Yesu alisema ***"mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake"*** **aya 38.** Ilikuwa ni katika mazingira ya ***"makutano walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji"*** **aya 36,** Yesu alichagua mitume kumi na wawili na akawatuma.

Akawaambia ***"katika njia ya mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli"*** **Mt 10:5-6.** Kuongea kwa kusisitiza, nyumba ya Israeli walifanana na Wayahudi wa siku hizo.

Kutumwa kwa wale sabini katika **Lk 10** ilikuwa pia ni kwa Wayahudi: nyumba ya Israeli. Kanisa la leo linaweza kusemekana kuwa kama 'nyumba ya Israeli'. Hii ni ya muhimu kwa kuwa leo kanisa linaishi kama mfano katika kila taifa. [Kuna makanisa yanayojificha katika mataifa ambapo hukumu ya kifo ndiyo adhabu kwa kuwa mmoja wa kukiri kristo].

Katika mazingira ya mwisho wa nyakati, 'kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli' ni mamilioni yasio hesabika ya waamini ndani ya Yesu ambao wamefungwa katika dini za kikristo na 'huduma huru' na makanisa. Wametawanyika na kuchoka na kama kondoo wasio na mchungaji. Hakika mavuno ni mengi lakini watenda kazi ni wachache. Huduma inahitajika kwa wingi kulileta kanisa katika ukomavu – wakati wa mavuno.

### Kuwahudumia Wasamaria na kisha kwa mataifa

Baada ya kufufuka, wakati Yesu alikuwa akiwaambia wanafunzi kuhusu kuja kwa Roho Mtakatifu, alisema, ***"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roha Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote*** [Wayahudi] ***na Samaria*** [Wasamaria], ***na hata mwisho wa nchi*** [kwa mataifa yote]***"* **Mdo 1:8.**

Ilikuwa kwanza ni kwa wayahudi, na wanafunzi wa kwanza walimtii Yesu katika kuisambaza injili katika Yerusalemu **(Mdo 1-7),** lakini walishindwa kwenda zaidi. Ilikuwa ni kwasababu ya mateso ambapo baadhi ya wanafunzi (Filipo) aliteremka Samaria kuhubiri (**Mdo 4:4-5**). Baadaye wengine wa wanafunzi hao waliotoka Yerusalemu kwa sababu ya mateso, waliihubiri injili katika Foineke na Cyprus, lakini wakiwahubiri wayahudi pekee.

Hata hivyo, katika Antiokia walianza kuwahubiria Wayahudi waliozungumza Kiyunani ***[Hellenists***] **Mdo 11:19-21**. Yesu alikuwa ameweka mpangilio: kwanza wanakondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli, pili, Wasamaria na tatu watu wa mataifa.

## YESU ALITUMANA MAVUNO MIONGONI MWA WASAMARIA

Mavuno haikuwa ipatikane tu kwa Wayahudi. Watenda kazi walipaswa kuondoka kuenda kwa mavuno Samaria. Katika **Yohana 4** Yesu alikuwa Samaria katika mji wa Saika. Hapo miongoni mwa Wasamaria Yesu akaongea tena kuhusu mavuno. Akasema, ***"hamsemi ninyi, bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, mimi nawaambieni, inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno"*** **aya 35.** Aliongea kwa wanafunzi waliokuwa naye kama kwa wale ambao watatenda kazi ya kuvuna Samaria. Kumbuka ***"Wavunaji ni malaika [wajumbe]",*** sio malaika kutoka mbinguni, lakini watenda kazi ambao Yesu anainua na kuwatuma.

Wasamaria walikuwa na mfano wa dini ya kweli ya agano la kale. Walimwamini Mungu **(Yn 4:20**) na walikuwa na matarajio fulani **aya 25**.

### Wasamaria ni akina nani?

Kihistoria, Wasamaria walikuwa ni watu ambao waliishi katika mji uliomilikiwa na Efraimu na makabila mengine ambao walihusisha ufalme wa kasikasini mwa Isaraeli. Ufalme huu ulikuwa umechukuliwa na Wasiria katika karne ya nane kabla ya Kristo. Watekaji walikuwa wamewachukua mateka wengi na walikuwa wamewaweka wengine katika nchi ya Israeli.

Wasamaria walikuwa ni ukoo wa jamii zilizotangamana. Licha ya historia yao ndefu ya kuwa walitekwa kutoka nyumba ya Isreli katika hali ya kuwa watu wa Mungu, walikuwa wamedumisha imani kiasi katika Mungu wa Kweli na wakawa na matarajio kiasi ya Masihi kama inavyoonekana katika picha ya mwanamke msamaria katika **Yn 4**.

### Wasamaria wanaweza kuwawakilisha akina nani leo?

Inawezekana kuelewa kwamba Wasamaria wanawakilisha vitengo vya kikristo. Vitengo vya kikristo wana mfano wa imani katika Mungu wa kweli na wana ufahamu kiasi wa Yesu,

Kristo. Kwa hivyo, kama yesu alivyosema katika **Yn 4**, mavuno miongoni mwa wasamaria yako tayari na mavuno leo miongoni mwa wale wanaopatikana katika vitengo vya kikristo iko tayari.

Kwa mfano mnamo 2009, nilipelekwa katika ofisi kuu ya kanisa kule Kenya ambayo wengi wanaitambua kuwa ni kitengo cha dini. Hata hivyo kwa siku mbili nilishiriki neno la Mungu na kikundi cha viongozi, wote wakuu na wadogo, na walilipokea neno la Mungu kwa furaha.

Kuna mlango uliofunguka kwa wahubiri wa Kikristo, mitume, na waalimu kuenenda katika vitengo hizi za dini katika Afrika ya mashariki, na pengine kuenenda katika vikundi vingine kama hivyo, kuwapelekea neno safi la Mungu na ujumbe ulio wazi wa injili ya Yesu Kristo.

## KUNA WATU WA MATAIFA AMBAO HAWAJAFIKIWA

Haikuwa mpaka wakati wa kufufuka kwake ambapo Yesu kwa kukusudia aliwatuma wanafunzi wake kwa mataifa yote: ***"basi, enendeni, mkawafanye mataifa wote kuwa wanafunzi wangu"* Mt 28:19a.**

Kuna wengi katika mataifa ambao hawajapokea shahidi mkristo. Ndugu zetu kule India wanatuambia 83% ya idadi ya taifa hilo kubwa wanaishi vijijini na kuwa vijiji 500,000 hawana ushuhuda wa Kristo [vijiji 100,000 wana shahidi]. Hakika kuna watu wengi ambao hawajafikiwa.

**Kazi ya uwanafunzi inaanza na kuihubiri injili lakini kazi ya uwanafunzi inaanza tu wakati mtu anaamini.**

### Baraza la Yerusalemu katika Mdo 15

Kwa sababu watu wengi wa mataifa walikuwa wanaitikia imani, kulikuwa na kutatanikiwa kwingi miongoni mwa wayahudi waamini kama mataifa wangeiweka sheria; kama walistahili kutahiriwa? Baraza la mitume na wazee waliitwa kutatua swala lile **(Mdo 15:6).** Baada ya ***"hoja nyingi"* aya 7,** baraza lilisikia kutoka kwa Petro, Paulo na Baranaba, na ***"mkutano wote wakanyamaza"* aya 12.** Yakobo akalileta neno kutoka kwa nabii Amosi lililotatua hoja, wakileta ufahamu kutoka kwa maandiko.

### Ilikuwa wakati wote ni kusudi la Mungu kuwafikia mataifa kupitia Masihi.

***"Baada ya mambo haya nitarejea, nami nitaijenga tena nyumba ya Daudi iliyoanguka. Nitajenga tena maanguko yake, nami nitaisimamisha; ili wanadamu waliosalia wamtafute Bwana, na mataifa yote ambao jina langu limetajwa kwao; asema Bwana ajulishaye hayo tangu milele"* Mdo 15:16-18.**

Urejesho wa hema ya Daudi haizungumzii hema ya kuabudu ambapo uwepo wa Mungu unadumu. Ila inazungumzia nyumba ya kifalme, ukoo, jamii ya viongozi ambayo ilianza na Daudi. Yakobo ananukuu kutoka **Amosi 9:11-12**. Kutajwa huku kwa hema ya Daudi sio kwa hema ambayo saduku la agano lilikaa. Ni onyesho ya jamii ya uongozi ambayo ilikuwa imepotea kutoka wakati wa uhamisho wa Babeloni. Hii ilikuwa ni hema 'Maskani' iliyokuwa imeanguka; ambayo ilikuwa imeharibiwa; na sasa ilikuwa inarejeshwa kupitia Masihi Yesu.

**Zaburi 2** inazungumza kwa nguvu kuhusu Masihi akitiwa taji kama mfalme wa Sayuni na akiyapokea mataifa yote kama urithi wake. Yesu Kristo ndiye Masihi! Yesu Kristo ndiye mwana mkuu wa Daudi ambaye alikuja katika utimilifu wa nyakati, pia akiwa Mwana wa Mungu. Kupitia injili ufalme wake unahubiriwa kwa mataifa yote.

### Mavuno miongoni mwa watu wa mataifa.

Yakobo alifahamu kwamba mavuno sasa yalikuwa yakiendelea miongoni mwa mataifa. Ushahidi ulikuwa washtua: Bwana alikuwa amemwaga Roho wake kwa watu wa mataifa hata kabla ya hao kubatizwa (**Mdo 10:44-47**). Walikuwa wamepokea kipawa kile kile kama wanafunzi siku ya pentekosti. Tangia wakati huo kwa nyumba ya Kornelio, mlango mkubwa ulifunguka kwa huduma kwa watu wamataifa katika mataifa mengi na miji. Mataifa mengi walikuwa wamekuja kwa imani ndani ya Yesu Kristo na walikuwa wakikua makanisani ambayo yalikuwa yameungwa na watu wa mataifa.

## TUNALILETA KANISA KATIKA UKOMAVU KWA NJIA GANI?

### Watenda kazi wanapaswa kufanya nini katika mavuno?

Maagizo ya Yesu yalikuwa ***"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza…"*** **(Mt 28:19a).** Kwa nini 'basi'? kwa sababu Yesu alikuwa amesema ***"nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani"*** **aya 18.** Tume ina msingi wa na katika kutoka kwa mamlaka ya Yesu duniani.

Yesu alikuwa akiongea katika kufufuka kwake. Alikuwa tayari ametoka kwa Baba yake. Alikuwa amekamilisha kazi ya ukombozi. Alikuwa amezitakasa mbingu kwa kuiweka damu yake katika kiti cha rehema (**Ebr 9:11-12, 24**), hivyo akihakikisha ukamilifu wa watakatifu (**Ebr 10:14**).

Sasa mitume ambao alikuwa ameandaa na kutuma walikuwa tayari kwenda kwa mataifa. Alikuwa akiwatuma kama watenda kazi katika mavuno.

Hata hivyo, mavuno ni zaidi ya uinjilisti, hivyo ni, kuihubiri injili kuzipata nafsi. Mahubiri hayo ya injili ni mwanzo.

**Lengo ni *"Kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo"* Kol 1:28b.**

## KAZI YA UWANAFUNZI

Zipo hatua sita ambazo mitume wa kwanza walichukua na tunapaswa kuufuata mfano wao.

1. **Hubiri injili, Mk 16:15.** Injili ni ya kila mtu. Injili ni ya watu wote, (**1Tim 2:6**). Ni mapenzi ya Mungu kwa ***"Watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli"*** **1Tim 2:4 [**pia **2Pet 3:9].**

   Tunapaswa kuhubiri: Yesu aliye Kristo, **Mdo 5:42**, ufalme wa Mungu na Jina la Yesu, **Mdo 8:12** na **Mdo 28:30**; utajiri usiopimika wa Masihi, **Efe 3:8**.

2. **Kuwabatiza wote walioamini, Mk 16:16a, Mt 28:19b.** Ubatizo unatakikana; sehemu muhimu ya wokovu. Ubatizo ni ***"kwa <u>jina</u> la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu"*** **(Mt 28:19b).** Majina ya biblia yalimaanisha yule mtu na mara kwa mara jina lilikuwa kiunabii likifunua tabia ya muhimu ya mtu huyo.

   Jambo muhimu hapa ni **jina.** Kubatiza inamaanisha kutumbukiza/kuzamisha. Kwa wepesi inaweza kuwa 'kuwaweka ndani ya **mtu** Baba Mwana na Roho Mtakatifu'. Huyu mtu ni nani? Wazi mtu huyo ni Yesu ambaye ni udhihirisho wa Mungu asiyeonekana, na jina lake ni Yesu. **Mdo 4:12** inatuambia ***"wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo".***

   Mitume walibatiza katika jina la Yesu. [ona **Mdo 2:38; 8:16; 19:5].**

3. **Kuwafundisha mambo yote ambayo Yesu ametufundisha, Mt 28:20.** Yesu alikuwa amewafundisha wale kumi na wawili kwa miaka mitatu na kwa ujasiri akawatuma kufundisha yale yote alikuwa amewafundisha. Twapaswa kufundisha:
   - Mafundisho ya kitume, **Mdo 2:42**
   - Kwamba Yesu ni Masihi, **Mdo 5:42**
   - Mambo kuhusu Bwana Yesu Kristo, **Mdo 28:31**
   - Mafundisho sawa, **Tito 2:1**
   - Kwa hekima yote, **Kol 1:28**
   - Twapaswa kuwafikishia wengine yale tuliyoyapokea, **2Tim2:2**

4. **Kudhihirisha ushirika wa kweli, Mdo 2:44-45** ***"na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa vitu vyote shirika…na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja".***
   Ushirika unahusisha kushirikiana kifedha na kwa hivyo waamini wapwa wanapaswa kufundishwa kutoa kulingana na maandiko – fungu la kumi na sadaka.

5. **Kumega mkate, Mdo 2:46.** Kanisa la kwanza walimega mkate ***"na siku zote…wakimega mkate nyumba kwa nyumba".*** Mitume walifundisha kwa udani maana ya kumega mkate katika **1 Kor 11:23-34**.

6. **Maombi, Mdo2:41-42.** ***"nao waliopokea neno lake wakabatizwa…wakawa wakidumu…katika maombi".*** Waamini wapya wanapaswa kufundishwa kuhusu maombi hata kama vile Yesu alifundisha maombi. Kwa hivyo twapaswa kufundisha ombi la Bwana kama mfano wa jinsi ya kuomba (**Mt 6:9-13 & Lk 11:1-14).**
   Wafundishe wanafunzi kuombea watu wote na walio kwenye mamlaka (**1Tim2:1-2**), na kuwaombea watakatifu ***"kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho"*** **Efe 6:18;** na kuwaombea mitume na wengine ambao wana majukumu ya kufundisha na kuhubiri neno la Mungu ili wawe na ujasiri ***"ili nihubiri kwa ujasiri ile siri ya injili"*** **(Aya 19).**

## Kutimiza tume

Tulipoenda India mapema februari, 2010, kufundisha katika washa ya wachungaji na viongozi, lengo letu lilikuwa ni kuwafundisha watakaofundisha wengine; kwa njia ingine, kuwaanda wachungaji na viongozi ili waweze kuwalea na kuwafanya wanafunzi waamini wapya.

Tulipoenda Filipino mwisho wa mwezi wa pili kufundisha katika washa ya wachungaji na viongozi, lengo letu lilikuwa 'kuliita kanisa katika ukomavu'.

Wakati Bruce na Jean Manning walienda India mwisho wa mwezi wa pili kufanya msururu wa washa ya wachungaji na viongozi, tena walikuwa wakifundisha wale watakaofundisha na kuita kanisa katika ukomavu.

Tulipoenda Afrika mwezi wa tano na wa sita 2010, katika mataifa matano, ulikuwa ni moyo wetu kuliita kanisa katika ukomavu kwa kuwaadaa watenda kazi kwa sababu ya kazi ya mavuno.

**BWANA wa mavuno ana mavuno mikononi**

Nilianza mafunzo haya ya mavuno kwa kueleza ndoto nilioota. Katika maandalizi ya fundisho hili niliota mara ya pili na katika ndoto nilikuwa na baba yangu wa asili – aliaga mwaka wa 1973. Baba yangu alikuwa ni mkulima wa ekali nyingi, akikuza nafaka.

Katika ndoto nilijua ni wakati wa mavuno lakini nilijihusisha na shughuli zingine kwa niaba ya baba yangu na nikajieleza hoja zangu kwake kuhusu mavuno yaliokuwa tayari. Baba yangu akanihakikishia ya kwamba alikuwa na mavuno mikononi na nisijisubue.

- ***Mungu asifiwe ya kwamba yeye ni BWANA wa mavuno.***
- ***Ni mavuno yake***
- ***Tunapaswa tumuombe***
- ***Atainua watenda kazi wa mavuno yake.***

# NGANO NA MAGUGU

### Kupokea nafsi sio mavuno.

Kwa miaka mingi, wengi wetu wameamini kwamba mavuno yanazungumzia kuleta nafsi katika ufalme wa Mungu. Nilipata kusikia kwa miaka kwamba wale ambao wamekuwa wakingojea siku za mwisho (matukio ya siku za mwisho) walitarajia mavuno ya nafsi ulimwenguni wote kabla ya mwisho wa nyakati. Imani hii ilianza kupokea changa moto miaka ya hivi punde, kama nilivyo soma na kufundisha Mfano wa Yesu wa ngano na magugu.

### Kuzipata nafsi ni mwanzo wa maisha ya ukristo

Mavuno katika lugha ya wakulima ni wakati ambapo nafaka ama tunda limeiva kwa sababu ya kuchuna ama kuvuna. Wakati mbegu inapandwa kwa shamba, tunaita hiyo ‘wakati wa kupanda’ na tunangojea chipukizi kutokea kutoka arthi. Wakati chipukizi mpya zinatokea mkulima anafurahia kwa sababu mimea imeanza kukua, lakini bado miezi minne ili ivunwe.

Kwa hivyo, kuzipokea nafsi katika ufalme wa Mungu hakika ni mwanzo mpya wa maisha ya mkristo na kuna wakati wa kukua ambapo mkristo anakua hadi ukomavu. Ni katika wakati tu wa ukomavu ambapo tunda linaanza kuiva. Huo ndio wakati wa mavuno.

Kwa hivyo tunapaswa kuuliza kama uinjilisti, hivyo ni kuleta nafsi mpya katika ufalme kupitia imani na ubatizo kama hakika ni mavuno ya mwisho wa nyakati ambayo maandiko yanazungumzia.

Hebu tuwe wazi: **kila maelezo ya mavuno lazima kimsingi ituambie ni wakati wa ukomavu na kupata mazao.** Mbegu ambayo ilipandwa imemea, imekua, imeleta mbegu kwa kichwa na mbegu imeiva tayari kwa mavuno.

### KANISA LINAPASWA KUJA KATIKA UKOMAVU.

Nafsi mpya hakika zinaonyesha ‘wakati wa kupanda’ sio wa kuvuna. Kwa hivyo kuleta nafsi mpya sio mavuno. Mavuno yanazungumzia wakati huo ambapo wana wa ufalme, wakiisha pandwa duniani wamekuwa katika ukomavu. Hayo ndiyo mavuno ambayo Yesu anazungumzia hata kama mimea katika shamba haivunwi mpaka nafaka imeiva, hivyo mavuno ya siku za mwisho ambayo Yesu anazungumzia, ni wakati ambapo kanisa, mwili ulio na sehemu nyingi, umekuja katika ukomavu katika ulimwengu, ukionyesha matunda ya haki.

Lengo la Mungu ni kanisa lake liufikie ukomavu, hata ukamilifu. Katika kupaa kwake, Yesu alitoa karama tano za huduma kwa ***“kuwakamilisha watakatifu”;*** alitoa karama za huduma zifanye kazi mpaka kanisa litakapoufikilia ukomavu, ***“hata kuwa mtu mkamilifu”*** **Efe 4:11-13.**

Katika **Ebr 6:1-3**, mtume tena anahimiza kanisa wakue. Anazungumzia kuhusu kuiweka misingi ya imani, lakini kusudi ni kanisa likue mpaka utimilifu: ***“tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu”.***

### Ni lazima tushike tafsiri ya mfano wa Yesu mwenywe

Katika **Mt 13** Yesu anafananisha mifano saba, miwili kati yao ni migumu kuliko mingine na hii miwili anaitafsiri. Ni ya muhimu kwetu sisi sote tushike tafsiri ya Yesu mwenyewe ya mifano yake.

Kwa mfano, wahubiri wengine wamesema kwamba mfano wa mpanzi na mvunaji ni kupanda ‘mbegu za pesa’. Tafsiri kama hiyo imepotoka mbali wakati Yesu mwenyewe alituambia ‘mbegu’ ni neno la Mungu.

## NGANO NA MAGUGU – MT 13:24-30

Yesu alisema *"ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake; lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake. Baadaye majani ya ngano yalipomea na kuzaa, yakaonekana na magugu.*

*Watumwa wa mwenye nyumba wakaenda wakamwambia, Bwana, hukupanda mbegu njema katika konde lako? limepata wapi basi magugu?*

*Akawaambia, Adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi, wataka twende tukayakusanye? Akasema, La; msije mkakusanya magugu, na kuzing'oa ngano pamoja nayo.*

*Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu".* **Uwanja**

## Tafsiri, Mt 13:37-43, Yesu alisema:

| | | |
|---|---|---|
| *Azipandaye zile mbegu njema* | *ni* | *Mwana wa Adamu.* |
| *Uwanja* | *ni* | *ulimwengu,* |
| *Zile mbegu njema* | *ni* | *wana wa ufalme,* |
| *Na yale magugu* | *ni* | *wana wa yule mwovu,* |
| *Yule adui aliyepanda* | *ni* | *ibilisi,* |
| *Mavuno* | *ni* | *mwisho wa dunia,* |
| *Wavunao* | *ni* | *malaika /wajumbe* |
| *Magugu yatakusanywa* | *ndivyo itakavyokuwa* | *Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi.* |
| *Na kuchomwa motomi* | | *na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndipo Kutakuwako kilio na kusaga meno.* |

*Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufame wa Baba yao.*
*Mwenye masikio, na asikie!*

### Mavuno ni wakati wa ukomavu

Kutoka kwa utafsiri ambao Yesu alipatiana wa mfano huu, ni wazi ya kwamba mavuno ni wakati wa mwisho, na ya kwamba katika wakati huo wa mavuno kile kilichokuwa kimepandwa kimekomaa. Wana wa Mungu wamekua katika ukomavu na wanadhihirisha haki yake ulimwenguni.

### Somo tulilojifundisha katika tafsiri ya Yesu

Utafsiri wa ngano na magugu ambao Yesu alipatiana, hakika inaleta changamoto nyingi za maono tofauti ya siku za mwisho

- Kwanza, inarekebisha kutofahamu kwetu kwa mavuno ni nini.
- Pili, inatufundisha wazi ya kwamba mavuno ni ukomavu.
- Tatu, ufalme wa mbinguni uko hapa duniani na hakika wana wa ufalme wamepandwa ulimwenguni ambapo ni lazima wakomae, tayari kwa mavuno.
- Nne, ni wana wa ibilisi watakaotolewa ulimwenguni na waangamizwe – hii ni tofauti sana na mafundisho ya kunyakuliwa ambayo inatwambia wenye haki wataondolewa ulimwenguni. Imefundishwa ya kwamba wenye haki watachukuliwa [kunyakuliwa]

kutoka ulimwenguni na waovu watatawala dunia kupitia serekali ya mpinga Kristo. Haya yanapingana na maneno ya Yesu mwenyewe.

- Tano, ni wavunaji ambao wametumwa na Yesu kuondoa waovu na wanaoasi kutoka ulimwenguni; matokeo yakiwa wenye haki watatawala ulimwenguni.
- Hatimaye, wakati waovu wataondolewa duniani, na ufalme wa Mungu umefunuliwa ulimwenguni, ulimwengu hapo utajazwa na haki ya Mungu.

## MALAIKA NDIO WAVUNAJI

Malaika katika Biblia inasungumzia wajube waliotumwa na Mungu. Lakini kuna malaika waovu vile vile, wanaowakilisha shetani na ni wajube wanadamu. Katika kiebrania na kiyunani, malaika na wajube wametafsiriwa kwa neno moja.

### Maana ya kamusi

Baadhi ya maelezo yafuatayo yametolewa kutoka kwa Strong’s Concordance na Vine’s Complete Expository Dictionary.

**SC Hebrew** # 4397 ‘*malak’* kutoka kwa mzizi usiotumika likimaanisha kutumwa kama mjube rasmi, linamaanisha mjube, haswa wa Mungu, hivyo ni malaika lakini pia nabii, kasisi au mwalimu. Imetafsriwa katika Agano la Kale kama: malaika (mara 111), mjube (mara 98), balozi (mara 4). Matumizi ya neno inategemea malaika aliyetumwa na Mungu, kwa mjube aliyetumwa na watu au mjube wa watu kutoka kwa Mungu.

**SC Greek** # 32 ‘*aggelos’* inatamkwa kama *‘angelos’.* Sawa na neno la Agano la Kale na kuwekwa katika Agano Jipya; limetoka kwa neno la msingi ikimaanisha ‘kuleta ujube’; inamaanisha mjumbe, haswa malaika wa Mungu lakini pia ikihusisha, mchungaji, [lakini pengine sawa sana mtume]. Malaika wa Mungu ni roho, hawana miili ya asili kama wanadamu, lakini malaika wanaonekana kwa jumla kwa mfano wa mtu. Malaika wa Mungu ni watakatifu.

### Chaguo la mtafsiri

Kutoka kwa ufahamu wa Kiebrania na Kiyunani na matumishi ya maneno yaliyotafsiriwa ‘malaika’ tunaelewa kwamba ni maamuzi ya watafisiri iwe watatumia jina ‘malaika’ ikimaanisha ‘mjumbe wa mbiguni’ ama kutumia jina ‘mjumbe’ ikimaanisha ‘mjumbe mwanadamu’.

Katika Agano Jipya kuna maeneo mawili kama sio matatu ambapo neno ‘malaika’ halifai kwa mazingira na shahidi wa maandiko mengine.

**Mfano wa kwanza: malaika kwa makanisa saba** katika **Ufunuo 1-3** haizungumzi kuhusu viumbe vya mbinguni visivyo na mwili. Hakuna ushahidi mwingine katika maandiko ambapo malaika wamechaguliwa na Mungu kulileta neno la Mungu makanisani. Hivyo wengine wamesema kwamba Yesu anazungumzia wachungaji, lakini hiyo haiafai maandiko pia, kwa maana wachungaji wametajwa mara moja (**Efe 4:11**) katika agano jipya.

Yesu aliwachagua nani kulileta neno la Mungu makanisani? Jawabu: mitume. Paulo alisema, ***“naliwekwa niwe mhubiri na mtume, nasema kweli, sisemi uongo, mwalimu wa mataifa katika imani ya kweli”* 1Tim 2:7.** Waandishi wote wa nyaraka ni mitume na waliyaandikia makanisa. Jambo ni hili kwamba wale ambao Yesu alichagua walileta neno la Mungu kwa kanisa la eneo ama mji walikuwa mitume. Kwa hivyo utafsiri ulio bora katika **ufunuo 1-3** inaweza kuwa ‘wajumbe’

**Mfano wa pili:** ***“Mwana wa Adamu atawatuma malaika/wajumbe wake”* Mt 13:41.** Katika utafsiri aliopeana Yesu wa mfano wa ngano na magugu, alisema kwamba wavunaji

watakuwa na majukumu makubwa katika siku za mwisho kuondoa ulimwengu wa wasio haki na wasio na Mungu.

Wakati Yesu alikuwa ulimwenguni, alikuwa akiwafundisha akina nani kuwa wajumbe wake? Kama ilikuwa ni viumbe vya mbinguni hakuhitaji kuja duniani kuwaandaa. Angewaandalia mbinguni. Hata hivyo tunajua jukumu la msingi la Mungu kama mtume wa Mungu ilikuwa kuwafundisha na kuwaandaa **mitume** ambao angetuma waende kwa jina lake, na mamlaka yake, kujenga kanisa na kuihubiri injili ya ufalme wa Mungu, hivyo ni, kuleta ufalme wa Mungu/mbinguni katika kudhihirishwa duniani.

**Mfano wa tatu:** ***"naye atawatuma malaika/wajumbe zake pamoja na sauti kuu ya parapada, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu"*** **Mt 24:31.** Wengi wetu wamedhania hii inazungumzia kazi kuu ya malaika katika dunia katika mwisho wa nyakati.

- Lakini Yesu aliwainua akina nani waihubiri injili?
- Aliwainua malaika waihubiri injili?
- Ni kazi ya malaika kuwakusanya wateule?
- Alituma akina nani wawahubiri wale ***"waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele"*** **Mdo 13:48?**

**Yesu aliwainua na kuwatuma mitume!**

## Wajumbe ni wapi ambao Yesu anatuma?

Katika Agano Jipya Yesu aliwatuma mitume. Alisema kwa Baba, ***"kama vile ulivyonituma (apostello – kutumwa kama mtume) mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma (apostello) hao (mitume) ulimwenguni"*** **Yn 17:18.** Kutamatisha kwenye maana kwa 'wajumbe ni wakina nani', ni kwamba wajumbe ni mitume.

Katika mwisho wa nyakati, Yesu tena anakiinua kizazi cha mitume ambao kupitia hao anazungumza neno lake kwa kanisa ulimwenguni kote na kupitia hao anaita wahuduma wake tena kuifanya kazi ya huduma kulileta kanisa katika ukomavu na utimilifu.

## Na kuhusu hukumu

Yesu alisema kwamba wajumbe wake ***"Watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi"*** **Mt 13:41.**

Wengi wamedhani hukumu katika mwisho wa nyakati itakuwa ya uharibifu ikipangwa na viumbe vya angani kwa niaba ya Mungu.

Hata hivyo, Yesu alisema kwamba atawatuma wajumbe wake na ***"watakusanya kutoka ufalme wake"*** wote watendao maasi. Wengi hawana maono ya mwili ulio na haki, uliojazwa na Roho unaozaa wa waamini waliokomaa, unaoitwa kanisa, hakika kuleta ushindi wa injili ulimwenguni na kuona ufalme wa Mungu ukiimarishwa.

Lakini Yesu ameketi ***"maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake"*** **1Kor.15:25.** Ni nani anayepaswa kuwaleta maadui wa Yesu chini ya miguu yake? Ni kanisa. Hukumu la wasio haki na waasi inakuja kupitia neno la Mungu.

**Kama kanisa katika ukomavu linaongea neno kwa uhakika,<br>ufalme wa Mungu utadhihirishwa ulimwenguni.**

Paulo anatuambia kwamba lengo la Mungu kwetu ni kutembea katika utiifu ambao ***"tukiwa tayari kupatiliza maasi yote"*** **2 Kor 10:6.** Hii inawezekana tu wakati tumeleta chini **ngome,** wakati tumeangusha **mawazo** na ***"kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu"*** **aya 4-5.** Hii inawezekana tu kwa nguvu za Mungu na matokeo yatakuwa ***"kuteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo".***

Hukumu ya Anania na Safira katika **Mdo 5,** kwa neno la mtume Petro, hakika ni mfano wa kutisha wa hukumu ya Mungu ikija juu ya kitu ambacho kilimchukiza Roho Mtakatifu. Hii ilikuwa ni katika kanisa na hukumu ***"huanza katika nyumba ya Mungu"*** lakini ***"mwisho wao wasiotii injili ya Mungu utakuwa aje?"*** **1 Pet 4:17; 2 The 1:8-9.**

## KUBADILISHA KWA MAWAZO

Ni ya muhimu kwetu kuchukua kwa kumaanisha utafsiri wa ngano na magugu tuliyopewa na Yesu. Ni ya muhimu kwetu kuyapatiana mawazo yetu na ufahamu wetu wa kusudi la Mungu mwisho wa nyakati kwa maneno haswa ya Yesu.

### Kupandwa ulimwenguni

Yesu anatupatia picha ya ajabu ya wana wa Mungu, wakiwa wamepandwa ulimwenguni, wakija katika ukomavu duniani. Tunda la wana wa ufalme wakikua katika ukomavu ulimwenguni haijaonekana na wengi kanisani kwa sababu kanisa limeanini mafundisho mabaya kuhusu mwisho wa nyakati. Waamini hawajahimizwa kukua katika uwana na kupandwa ulimwenguni kama wana wa ufalme. Kanisa limekuwa ngome katika jamii na wakristo wanajiondoa katika ngome hiyo kwa ujuzi wao wa maisha ya kanisa.

### Kuamini injili kamili

Katika siku hizi za urejesho, Yesu anawarejesha mitume na huduma zote tano kanisani lake kwa kusudi lile la kulileta kanisa katika ukomavu. Zaidi na zaidi ya watakatifu wa Mungu wameanza kuisikia injili ya ufalme wa Mungu; wanaanza kutambua kuwa kuna mengi zaidi katika wokovu ambao Mungu ametuitia kuliko kuokolewa na kwenda mbinguni.

### Kuwafanya wanafunzi

Tunapofanya kazi ya huduma kwa uaminifu, ambayo kimsingi ni kuwafanya wanafunzi ambao wanaweza kufundishwa kufanya kazi ya huduma na kutumwa duniani, tunayaona matokeo ambayo maandiko yanazungumzia.

Katika SHILOH, tumejipatiana katika kuwafanya wanafunzi na kuwaandaa watu watoke na waende katika mavuno. Tumejipatiana katika kumuandaa kila mshirika na tunayaona matokeo kama zaidi na zaidi wandugu wanapoenda kuwafundisha wengine; wanaenda kwa huduma Australia na mataifa ya ng'ambo.

# UHAKIKA WA KUNYAKULIWA

## SEHEMU YA KWANZA

# MAFUNDISHO YA KUNYAKULIWA YALITOKA WAPI?

### Mawazo ya kanisa 'likinyakuliwa' ni ya hivi karibuni katika historia ya kanisa

Kwa zaidi ya karne moja wengi wamehubiri na wamefundisha kunyakuliwa kwa kanisa kwenda mbinguni kwa kipindi cha miaka saba (wengine wanasema miaka tatu na nusu). Imani katika kunyakuliwa inaweza onekana ikiwa ya dunia yote katika vikundi fulani. Kwa mfano, baadhi ya viongozi wa wakristo kutoka India ambao walihudhulia mafundisho ya shule SHILOH Australia, walisema hawajawahi kusikia kitu tofauti na kunyakuliwa ikiwa ndio hatma ya kanisa.

Hata hivyo kuna mwili unaokua wa waamini, wahubiri, na waalimu, ambao hawaamini katika 'kunyakuliwa'. Wengine wamekua makanisani ambapo mafundisho ya kunyakuliwa hayajasikika; wengine watubu baada ya kujitoa katika kusoma Biblia kwa makini.

### Kunyakuliwa kwanza kulihubiriwa mwaka wa 1820

Mawazo ya 'kunyakuliwa' ilikuwa haijulikani katika historia ya kanisa. Nukuu ifuatayo ni kutoka kwa kitabu cha Iain Murray, Puritan hope, kilichoandikwa mwaka wa 1971 na kuchapishwa na Banner of truth trust;

***'imani yenye shauku la kujua, ambayo haijulikani katika historia ya kanisa iliinuka, iliyoitwa, kwamba kuja kwa Yesu kabla ya miaka 1000 itakuwa katika vipindi viwili, cha kwanza, kunyakuliwa kisirisiri kuliondoa kanisa kabla ya dhiki kuu kugonga dunia, ya pili kuja kwake na watakatifu wake ili kuuimarisha ufalme wake'*** **(Ukurasa 200).**

Matarajio kwamba kutakuwa na unyakuzi wa kanisa kabla ya 'dhiki kuu', ikiingia katika kipindi{i}; kabla ya milenia{ii}; picha ya mafundisho na imani, ilikuwa haijulikani katika historia ya kanisa kabla ya 1820.

{i} *Kipindi: inazungumzia mpangilio wa kufahamu utendaji wa Mungu katika Historia ya Mwanadamu. Mpangilio huu uliwekwa na muanzilishi mmoja wa mafundisho ya kunyakuliwa, J N Darby, na kwa nguvu akafundisha katika Scofield Reference Bible iliyotolewa mapema katika karne ya ishirini. Ufahamu huu wa maandiko yenye mpangilio ya kipindi hiki ni mawazo mengi ya fikira za mwanadamu na utafsiri juu ya neno la Mungu kama lilivyoandikwa.*

{ii} *Kabla ya miaka elfu moja: inaongea juu ya ufahamu kwamba Yesu atarudi duniani kabla ya 'utawala wa miaka 1000 iliyotarajiwa' wa Kristo duniani; imetolewa katika mambo yalioonyeshwa katika kitabu cha ufunuo (**Ufu 20:2,3,4,5,6,7**). Mtazamo wa kihistoria wa kutajwa kwa miaka elfu moja, ni kwamba sio muda uliowekwa, haswa kwa sababu kutajwa kwa miaka 1000 imetajwa katika kitabu cha ufunuo. Kitabu cha ufunuo kimeandikwa katika lugha ya kinabii, maono na matukio kwa sababu ni kitabu cha ufunuo, kwa jumla ili kitafsiriwe, sio kuchukuliwa kama kilivyo, na kinatakiwa kueleweka kupitia Roho, sio kwa mawazo ya mwanadamu.*

### Historia ya elimu ya kunyakuliwa

**Mr Edmund Shackleton**i *alikifungua kitabu chake kwa msemo, "wote walioshikilia kuja kwa Kristo kabla ya kuja miaka elfu moja walikuwa…wa mawazo moja katika jambo hilo"*

*(mpaka 1830). Kwa wakati huo mtazamo mpya ulianzishwa kwamba kuja kwa Yesu* ***haikuwa tukio moja, lakini kwamba ilikuwa imegawanywa katika ngazi.*** *Ilianza kufundishwa kwamba Kristo atakuja mara mbili kutoka mbinguni mpaka duniani, lakini mara ya kwanza atafika tu hewani.*

*Kushuka mara ya kwanza, inasemekana, itakuwa ni kwa kusudi ya kulihamisha kanisa duniani, na utatendeka kabla ya dhiki kuu chini ya mpinga kristo. Hii inaitwa 'kuja kwa watakatifu wake' au 'kunyakuliwa kisirisiri'.*

*Sehemu ya pili ya kuja inasemwa itatendeka wakati Kristo atakapokuja katika utukufu na aharibu mpinga Kristo. Hii inaitwa, 'kuja na watakatifu'.*

**Mr. H.A. Baker** aliandika, "*kwa karne 18 kanuni za msingi ya* ***dhiki kwa utukufu*** *ilikuwa imani ya ulimwengu wote wa washirika wa kanisa walio zaliwa tena hakika".* H.A. Baker alisema "*ilianzia na mwanamke wa Irvingite, kisha ikaendeshwa na Jonn N.Darby karibu 1830, mafundisho haya mapya yametufikia mpaka ikajulikana. GEORGE MULLER aliipinga; vivyo hivyo alifanya Benjamin Wills Newton; vivyo hivyo alifanya Dr. S.P. Tregelles na wapendwa wengine"*

**Dr. Oswald J. Smith** alisema, *"mafundisho mapya ya Kabla ya Dhiki yalitangazwa kwanza kama ufunuo wa moja kwa moja na mwanamke katika kanisa la Edward Irving, na kisha ikachukuliwa na John Nelson Darby (na Scofield Refrence bible) katika kutatanikiwa wazi kwa mafundisho ya kanisa kwa miaka 1800).*

## KUNYAKULIWA KATIKA BIBLIA

### Neno 'kunyakuliwa'

Neno kunyakuliwa **halionekani** katika Biblia ya kingereza. Ni jambo la kushangaza kutambua kwamba baadhi ya elimu ambayo imeshikiliwa kila siku na wakristo wengi, ikihusisha wasomi wa Biblia, hayajapatikana kwa jina katika Maandiko Matakatifu. Ambacho wahubiri na waalimu wamekuwa wakifanya ni kukubali mafundisho na kwenda kwa maandiko kudhibitisha mafundisho hayo. Hii ni kinyume kabisa cha thiologia ya kweli ya Biblia. Mafundisho yote ya kweli lazima yatokee wazi kutoka kwa maaelezo katika Maandiko, na yadhibitishwe katika Maandiko.

Oxford dictionary inasenma: ***kunyakuliwa*** inamaanisha *kuhamisha mawazo, thiologia ya kusisimua na kufurahisha, kitendo cha kusafirisha mtu kutoka eneo moja hadi ingine [haswa mbinguni]*. Neno hili limetoka kwa Latin '***raptura'*** na neno linalotumika katika ukristo inatoka kwa Biblia ya Latin.

Aya katika Biblia ambayo wote ambao wanaamini katika kunyakuliwa hutumia kama dhibitisho ya msingi wa mafundisho kama hayo [matukio kama hayo yakitekelezwa] ni **1The 4:17**. ***"Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele".***

Neno la *kunyakuliwa* ni ***harpadzo*** Strong's Concordance [SC]
Kiyunani #726 ikimaanisha: *kukamata kwa nguvu, kunyakua, kuinua juu, kuchukua kwa nguvu.*
Neno linaeleza kitendo ambacho Roho Mtakatifu alimhamisha Filipo kutoka eneo moja hadi lingine (**Mdo 8:39**) na paulo akichukuliwa mpaka paradiso (**2 Kor 12:2,4**). Inaeleza kitendo cha nguvu za ghafla na inatumika katika **Mt 11:12**.

[*Word Wealth in New Spirit Filled Bible*, **1 The 4:17**].

Maana ya neno *harpadzo* inaleta mwangaza ama ufahamu wa yale yalitendeka wakati Bwana Yesu alishuka kutoka mbinguni. Neno la kiyunani halionyeshi kwamba tutachukuliwa mbinguni, lakini tutanyakuliwa kumlaki Bwana hewani, ajapo, kama vile maandiko yasemavyo.

Kwa sababu ya matumizi mengi ya neno, tunaweza kufahamu ya kwamba tutanyakuliwa kwa njia ya kiungu kutoka duniani na kumlaki Bwana hewani. Hatutaweza kumpinga.

#### Neno la '*kuchukuliwa juu'*

Ni ajabu ya kwamba neno la kuchukuliwa juu (mbinguni) ambalo hutumika katika **Mdo 1:2, 11, 22,** katika **Mariko 16:19, Mdo 10:16** na katika **1Tim 3:16** [kupokelewa juu NKJV], ni neno ***analambano*** SC Gr 353 ambayo inamaanisha: *kuchukuliwa juu.*

Hii ni neno tofauti sana kwa neno ***harpadzo*** ambayo inamaanisha ***kunyakuliwa*** katika **1The 4:17**. Kunyakuliwa katika aya hii ni kukutana na Yesu hewani. Hakuna maana ya kuwa neno hili limemaanisha kuchukuliwa mbinguni.

#### Neno 'kuja'

Neno la <u>kuja</u> ni ***parousia*** SC Gr. #3952 ikimaanisha:

- *Kuwa karibu, hivyo ni, kufika [*mara kwa mara kurudi; haswa kwa Kristo kuadhibu Yerusalemu au waovu].

Neno hili limetoka Gr. #3918 ikimaanisha: *kuwa karibu, hivyo ni, mkononi.*

- Neno haswa likionyesha kuja kwa Yesu mara ya pili, halijawahi kutumika kuonyesha kuja kwake mara ya kwanza, lakini lilikuwa likionyesha '*uwepo wa Kristo na wanafunzi wake kwenye mlima wa kubadilishwa'* **2 Pet 1:16.**

***Parousia*** mwanzo ilikuwa ni neno rasmi la kutembea kwa mtu mwenye mamlaka ya juu, haswa mfalme. **Ilikuwa ni kufikika ambayo ilihusisha kudumu kwa mtu huyo kutoka wakati wa kufika na kuendelea.** Kufika kwa Masihi mwenye utukufu kutafuatwa na kudumu kwake kwa milele na watu wake waliotukuzwa. [*Word Wealth in New Spirit Filled Life Bible,* **1Kor 15:23***; na kutoka SC Gr Dictionary]*

## KANISA LITAPITIA MATESO

### Kabla ya mateso kuja

Kanisa la agano jipya halikufundisha kunyakuliwa, hata halikufundisha kuja kwa Yesu Kristo kabla ya utawala wa miaka elfu moja kabla ya mateso. Katika **Mt 24:15-16**, Yesu anawaonya wanafunzi kwamba ***"mtakapoliona chukizo la uhalibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli… ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani".*** Luka anaiweka kwa njia wazi, ***"lakini, hapo mtakapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, ndipo jueni ya kwamba uharibifu wake umekaribia. Ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani…"*** **Luka 21:20-21.** Uharibifu hakika ulikuwa ni Jeshi la Kirumi wakizunguka Yerusalemu {iii} na mwisho kuchukua mji, ikihushisha uharibifu wa hekalu la Yerusalemu

{iii} *Ni vema kwetu kuwa na ufahamu kiasi wa uharibifu wa Yerusalemu katika mwaka wa AD 70 kama Yesu alivyotabiri kwa mitume katika* ***Mt 24, Lk 21*** na ***Mk 13.*** *Kutoka wakati wa kifo cha Yesu wayahudi, haswa walioishi katika wilaya ya Judea Rumi, walikuwa katika magombano ya kuendelea na watawala wao wa kirumi. Kuna wengi walioinuka; masihi wa uongo waliinuka na wakakusanya vikundi zilizokuwa na silaha kupinga Rumi, na ukawa ni wakati wa utata sana. Kiongozi wa kirumi akaagiza majeshi yake kukabiriana na wayahudi walioasi. Hii ikaleta uvamizi wa Yerusalemu na Jeshi la kirumi.*

*Haya ndiyo haswa Yesu alikuwa amewaonya wanafunzi wake kuhusu, na akasema 'mkiona haya yakitendeka mtoroke'. Wakristo waliyashika maonyo na wakaweza kutoroka Yerusalemu wakatorokea pahali panaitwa pella. Waliweza kutoroka kwa sababu katikati ya uvamizi ule, uvamizi ulisitizwa kidogo kwa mda kidogo. Kwa maana kiongozi aliyeongoza uvamizi ule aliitwa arudi Rumi. Uvamizi ulirejelewa kwa nguvu na mji ukavamiwa na kuharibiwa. Wahistoria wanakisia zaidi ya wayahudi 1,000,000 walikufa wakati huo wa hofu.*

*Myahudi mhistoria, Josephus alikamatwa katika uvamizi huo na akaruhusiwa atoroke na uhai wake na warumi na ameelezea ujuzi wa matukio katika maandishi yake.*

Katika kifungo hicho katika **Mathayo**, kisha Yesu anaonya ***"kutakuwapo dhiki kubwa"* (24:21).** Anasema "***na kama siku hizi zisingalifupizwa, asingeokoka mtu yeyote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo" Aya 22.*** Ni wazi kutoka kwa kitengo hiki kwamba wateule watajidhibiti dhiki kuu, sio kwa kuchukuliwa mbinguni katika misheni spesheli ya kunusuru, lakini kwa Bwana akiwahifadhi wakati wa dhiki. Yesu alisema kwamba Mungu atawaangalia wateule wake na afupishe **siku za dhiki.**

Yesu tayari alikuwa amesema ***"lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye ataokoka"* (Mt 24:13).** Kanisa limeitwa "***kuvumilia hata mwisho"!*** Kanisa limeitwa na kutumwa lifanye wanafunzi mpaka ***"ukamilifu wa dahari" (Mt 28:20).*** Yesu alisema ***"mimi nipo pamoja nanyi sikusote, hata ukamilifu wa dahari",*** mnapoenda na kufanya wanafunzi **(Mt 28:19-20**).

### Kuhifadhiwa katika dhiki

Katika kuliandikia kanisa la Wathesalonike mara ya pili, Paulo analiandikia kanisa ambalo lilikuwa linapitia adha na dhiki kwa wakati huo; ***"kwa ajili ya saburi yenu na imani mliyo nayo katika adha zenu zote na dhiki mnazostahimili"* 2 The 1:4.** Paulo anatumia nafasi hii kulihimiza kanisa, kwa kuwaambia kwamba Mungu atawahifadhi kupitia dhiki na mwisho kulipatia kanisa raha ***"wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni, pamoja na malaika wa uweza wake; katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu"* (2The 1:7-8.)**

Paulo haliambii kanisa kwamba Yesu ataingilia na kulichukua kanisa na kulipeleka mbinguni liondokee adha na dhiki. Ila analiambia kanisa kwamba saburi yao na imani katikati ya mateso *"**Ndiyo ishara hasa ya hukumu iliyo haki ya Mungu, <u>ili mhesabiwe kuwa mwastahili kuingia ufalme wa Mungu,</u> ambao kwa ajili yake mnateswa"*** **(2 The 1:5)**

### Mateso na Dhiki

Katika **2The 1:4-5**, kanisa lilikuwa likipitia dhiki na mateso na neno la Mungu linaahidi kwamba watesi wa kanisa watalipwa kwa ***"dhiki"*** **aya (6).** Kusoma sawa kwa aya hii ni kwamba kanisa lilikuwa likipitia dhiki; walikuwa wakiteswa. **Kanisa la sasa linastahili kuandaliwa kwa adha na dhiki,** kama halijafanya hivyo, [kama China ambapo kanisa limepitia dhiki kuu na mateso kwa zaidi ya miaka 55]

Kanisa linakombolewa kutoka dhiki hii ***"wakati Bwana Yesu atafunuliwa kutoka mbinguni".*** Anafunuliwa kutoka mbinguni na malaika wake wakuu "***katika mwali wa moto, huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu" aya 8.*** Hii ni baada ya dhiki, sio kabla!

## Tunaingia ufalmwe kupitia dhiki

Baada ya kulipanda kanisa katika Listra na Ikonio, Paulo na Baraba walikuwa wakirudi kutoka kwa safari yao ya kitume ya kwanza, wakitembelea tena makanisa, walikuwa ***"wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile imani, na ya kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi"*** **(Mdo 14:21-22).** Kwa kusikitisha sio wengi leo wanaozifanya **imara roho za wanafunzi',** sio wengi wanaoliandaa kanisa kwa dhiki ambayo haina budi kutokea, hivyo ni, wakati wa kuteseka na kudhihakiwa.

Wachungaji na wahuduma ambao wanaamini katika mateso kabla ya kunyakuliwa hawaamini wala hawaelewi ushindi wa injili na kushangilia kwa kanisa la Yesu Kristo hapa duniani. Ushindi na kushangilia zimewekwa mbali hata wakati ujao wa 'miaka elfu'. Wahubiri kama hao wanaona kusudi tu la kanisa duniani leo ni kujitayarisha kwa kunyakuliwa.

Kumbuka kunyakuliwa haionekani kwa maandiko, lakini maandiko mengi yamenukuliwa kutoka hapo na hapo kuliunga wazo kama hilo, kwa kufanya hayo, maandiko yanatolewa kutoka kwa mazingira, na jambo la muhimu la injili na kusudi la Mungu, duniani halijaeleweka, hata pengine limepuuzwa.

# UHAKIKA WA KUNYAKULIWA?

## SEHEMU YA PILI

# KUFUFULIWA WAFU

### Kufufuliwa wafu: fundisho kubwa

Fundisho kubwa ya Agano Jipya na fundisho la msingi wa imani yetu ni elimu ya kufufufliwa wafu. Duniani kote, kanisa la Bwana limepuzilia katika kufundisha elimu ya msingi [soma kwa makini **Ebr 5:12-6-3**]. Lakini hata baya zaidi kuliko haya, sehemu kubwa ya kanisa imechukulia elimu ya mwanadamu: 'kunyakuliwa kwa kanisa' badala ya elimu ya kufufuliwa wafu.

Tumaini haswa la kufufuliwa limechukuliwa na wazo la kufurahisha kwamba tutasafirishwa mbinguni kwa miaka saba kwa kunyakuliwa kisirisiri. Elimu hii haina msingi imara katika maandiko, lakini imetiliwa maanani sana kwamba waamini wengi wameipokea elimu hii na wakakana uhakika wote wa muhimu wa kufufuliwa wafu.

### Kunyakuliwa: ilitoka wapi?

Neno *kunyakuliwa* halipatikani katika Biblia ya kingereza. Zaidi neno lilikuzwa kutoka kwa Biblia ya kikatoleki ya Latin. Kwa hivyo mazingira ya **1The 4:13-18** ni kuhusu kufufuliwa wafu. Kwa hivyo ina undanganyifu mwingi kwa waandishi na waalimu kuingiza neno 'kunyakuliwa' katika aya hizi wakati aya hizi zinaelezea kufufufuliwa wafu.

Haya ndiyo yanatendeka tukizifuata elimu za wanadamu: tunaacha mafundisho muhimu ya msingi ya injili na Biblia na kupindua maandiko ili tuunge mafundisho mapya ya kusisimua kama ya kunyakuliwa. Kufufuliwa wafu ni elimu ya muhimu na ya msingi wa imani

Kifungu hiki katika **1Wathesalonike** hakina jambo la kusema kuhusu kurudi mbinguni na Yesu, lakini wazi inasema ***"tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani".*** Hii inazungumzia **kufufuliwa kwa mwili!**

### KUJA

### Kuja kulingana na 1 Wathesalonike

Hebu tuangalie kwa makini katika **1The 4**. Mstari muhimu wa eskatologia ya unyakuo {iv} ni **aya 17**: ***"kisha sisi tulio hai tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele".*** Aya hii ni ya muhimu kujifundisha katika haki yake lakini pia kujifundisha katika mazingira ya kifungu ambacho inatokea.

{iv} ***eskatologia****: mafundisho ya unabii wa siku za mwisho na matukio. Mafundisho haya ni ya kutatanisha sana na kuna kutokukubaliana kwa jumla kuhusu mitazamo tofauti tofauti ya yanayofundishwa kama elimu ya siku za mwisho. Kama vile mtu mmoja alisema, 'kama ukiwakaribisha walimu kumi na wawili wa elimu ya siku za mwisho kutoka vyuo kumi na viwili vya Biblia waje wote kwa washa na kila mmoja afundishe, kutakuwa na mitazamo tofauti kumi na miwili'.*

## Waliolala mauti

Kifungu kimetangulizwa katika **aya 13**, ambapo Paulo anazungumzia swala la waamini [waliopendwa] ambao "***wamelala mauti",*** hivyo ni walio kufa katika imani. Paulo hataki tusijue. Anasema "***ikiwa twaamini kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye" aya 14.*** Tunajifundisha katika aya hii kwamba wale waliokufa ndani ya Kristo watakuja na Yesu – Mungu atawaleta pamoja naye atakapokuja! Ni wazi: wakati Yesu atakapokuja **wafu ndani ya Yesu** watakuja pamoja naye.

## Wafu watafufuliwa

Kufufuka kwa Yesu katika wafu ndio jambo muhimu au msimamo wetu katika imani yetu na, kwa maana Yesu Kristo alifufuka katika wafu, tunatazamia kufufuliwa wafu. ***"Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala [walio kufa]"*** **1Kor 15:20.** Hii inamaanisha kwamba kufufuka kwa Yesu ndio hakikisho la jambo la ajabu sana: kwa sababu alifufuka katika wafu, kufufuliwa kwetu kumehakikishwa.

***"Lakini kama hakuna kiyama ya wafu, Kristo naye hakufufuka"*** **1Kor 15:13.** Kufufuka kwa Yesu Kristo ndiyo hakikisho ya kwamba wafu watafufuka. ***"Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka"*** **aya 16.**

Imani yetu ina msingi katika kufufuka kwa Yesu. ***"Na kama Kristo hakufufuka, imani yetu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu"*** **aya 17.** Hakuna tumaini kwa waamini ambao wamekufa kama hakuna kufufuliwa wafu. ***"Na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea"*** **aya 18.**

# KUFUFULIWA

## Fundisho ya msingi

Kufufuliwa wafu ni elimu ya msingi ya imani ya wakristo. Ni mojawapo ya kanuni za msingi zilizonakiliwa katika **Ebr 6:1-2**. Hapana mahali popote katika maandiko ambapo kunyakuliwa kumetajwa. Hakika sio elimu ya msingi, na isitatanishwe na elimu iliyofunzwa vyema ya kufufuliwa wafu.

Kila mwamini anapaswa kufundiswa ***"mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu"*** **Ebr 5:12.** Kuna kanuni sita za misingi zilizonakiliwa katika **Ebr 6:1-2**. Hatupaswi kubaki tukiwa watoto wachanga, wala kubaki tukiwa watoto ***"tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu"*** **Efe 4:14.** Wengi wamefundishwa elimu ya kunyakuliwa lakini wanajionea katika maandiko. Kama matokeo wamekuwa na shaka ya uwezo wao wa kusoma maandiko kwa sababu wanadhania kwamba waliowafundisha mafundisho ya kunyakuliwa wamehitimu ***"kutumia kwa halali neno la kweli"*** **(2Tim 2:15).**

## Tumaini

Kufufuliwa wafu ndiyo tumaini la kanisa sio 'kunyakuliwa' mda kidogo kwenda mbinguni. Kufufuliwa kwa mwili ni kwa umilele. Pasina tumaini la kufufuka, ambapo msingi wake umeimarishwa katika uhakika wa kufufuka kwa Yesu katika wafu, imani yetu ni bure. [*tafadhali soma tena kifungu chote cha* **1Kor 15:12-19**].

Wale ambao hawaelewi kufufuliwa wafu wanaiacha kando na kubadilisha tumaini la kufufuliwa na tumaini la wakati mndogo la kunyakuliwa, wakindanganya kanisa kuwa na tumaini la uongo.

Wengi wanauliza maswali kuhusu siku za usoni baada ya Bwana amekuja. Maswali kama hayo ni vigumu sana kuyajibu. Yohana anasema, ***"wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala***

***haijadhirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo"*** **1 Yn 3:2.**

### Kufufuliwa inatendeka lini?

Kufufuliwa kwa mwili kunatendeka wakati Bwana Yesu atashuka kutoka mbinguni na tutamlaki hewani! Hii ni ya muhimu:

**kufufuliwa wafu inatendeka atakapokuja Yesu**

Biblia inasema kwamba ***"maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa. Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo <u>atakapokuja</u>"*** **1Kor 15:21-23.**

Sio tu wafu katika Kristo watafufuka, lakini ***"sisi tulio hai tuliosalia"*** pia tutafufuka (**1The 4:17).** Tunapaswa kufarijiana kwa tumaini hili (**aya 18**).

Ni wakati atakapokuja Yesu na 'kunyakuliwa' pamoja na wafu katika Kristo, ambao wanakuja na Kristo kutoka mbinguni kuipokea miili yao mipya, ambapo tutakaokuwa hai tutapokea miili yetu ya 'ufufuo'. Miili ya ufufuo itaishi milele; haitaona mauti tena, ***"Tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena"*** **Rum 6:9.**

### Kufikia ufufuo

Paulo alitamani ***"kufikia kiyama ya wafu"*** **(Flp 3:11).** Alitamani kufanya chochote, kulipa kila gharama ili afikie. Pia hapajatajwa kunyakuliwa kuwa tumaini lake au hatima, lakini kumjua Yesu ***"na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake"*** **Flp 3:10.** Huu ni ukristo tofauti sana kuliko tunaoujua, unaozungumzia ufanisi, mitindo ya kisasa ambayo imeshika maisha ya kanisa katika mataifa ya magharibi.

## WAFU KATIKA KRISTO

### Wako wapi wafu katika Kristo sasa?

Kwa hivyo tunauliza swali: wako wapi wafu katika Kristo sasa? Kama wanakuja na Yesu wakati atakapokuja, basi lazima wawe mbinguni katika miili yao ya roho. Hii imeelezwa vizuri katika **aya** ya **14 (1 The 4**).

Hii inathibitishwa katika **2 Kor 5:6 & 8, "*wakati tuwapo hapa katika mwili, tunakaa mbali na Bwana…nasi tunaona ni afadhali kutokuwemo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana".***

<u>*Wakati mkristo anakufa katika imani, anaenda kukaa na Yesu mbinguni,*</u>
<u>*wanangojea kuja kwake, kwa maana watakuja naye.*</u>

### Kwa neno la Bwana

Katika **1 The 4:15**, Paulo anahimiza, ***"kwa kuwa tunawaambieni kwa neno la Bwana".*** Paulo ana uhakika! Anataka tujue ya kwamba siri ambayo ako tayari kuifunua ni ufunuo ambao ameupokea '**kwa neno la Bwana'.** Sio maoni ya Paulo; hakujifundisha elimu hii kutoka kwa mtu mwingine.

- Jambo litatendeka ***"wakati wa kuja kwa Bwana";***
- Itawahusisha waliokufa katika Kristo;

- Itawahusisha waumini walio duniani ambao wanatazamia kuja kwake.
- Kutakuwa na kizazi cha waamini [watakatifu] watakaokuwa hai wakati Bwana Yesu atakapokuja.
- Lakini kuja kwake kunahusisha kuja ***“pamoja naye waliolala katika Yesu”*** **Aya 14.** Mungu atawaleta pamoja na Yesu wakristo wote waliokufa na wako na yeye katika himaya ya mbinguni.

## Kufufuliwa kwa mwili

Waliokufa ndani ya Yesu Kristo hawako kaburini kama wengine wanavyofundisha kimakosa; wako na Yesu mbiguni katika miili yao ya roho. Tuna mwili wa asili na mwili wa roho na nafsi yetu imeunganishwa au sehemu ya mwili wetu wa roho. Wakati mtu anakufa ni mwili wa asili ambao unakufa.

Nafsi ya mtu ambayo imeunganishwa na sehemu ya roho ya mtu imeumbwa kwa umilele. Paulo anaiweka wazi katika aya hizi katika **1 The 4:13-14** na **2 Kor 5:6-8** kwamba wafu katika Kristo wako na Bwana sasa na kuna ufufuo unaokuja wa miili yao, lakini mwili utakaofufuliwa utakuwa mwili wa utukufu.

## Ufufuo utakaokuja

Baadhi ya aya katika **1Kor15:35-49** inatusaidia kufahamu hatima ya kufufuka katika mwili:

- ***“Lakini labda mtu atasema, ‘wafufuliwaje wafu? Nao huja kwa mwili gani?’*** **Aya 35**
- ***Ewe mpumbavu! Uipandayo haihuiki, isipokufa”*** **Aya 36.**
- ***“Lakini Mungu huipa mwili kama apendavyo, na kila mbegu mwili wake”*** **Aya 38.**
- ***“Kadhalika na kiyama ya wafu. Hupandwa katika uharibifu; hufufuliwa katika kutokuharibika; hupandwa katika aibu; hufufuliwa katika fahari; hupandwa katika udhaifu; hufufuliwa katika nguvu; hupanda mwili wa asili; hufufuliwa mwili wa roho. Ikawa uko mwili wa asili, na wa roho pia uko”*** **Aya 42-44.**
- ***“Na kama tulivyochukua sura yake yule wa undongo, kadhalika tutaichukua sura yake yeye aliye wa mbinguni”*** **Aya 49.**

# UHAKIKA WA KUNYAKULIWA?
## SEHEMU YA TATU

## YESU ATASHUKA KUTOKA MBINGUNI

**“*Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni”* 1The 4:16.**

- Yesu atashuka kutoka mbinguni – kushuka inamaanisha *kuja chini.*
- Yesu amepokelewa mbinguni “***hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote’* (Mdo 3:21)**
- Yesu aliongea kinabii kuhusu kuja kwake akisema “***akija juu ya mawingu ya mbingu”* (Mt 26: 64, Mk 14:62, Mt 24:30).**

### Atakuja jinsi alivyoenda

Malaika wakaambia wanafunzi ***“huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, <u>atakuja jinsi iyo hiyo</u> mlivyomwona akienda zake mbinguni”* Mdo 1:11.**

***“Akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao”* aya 9.** Kwa hivyo atakuja duniani kwa mawingu.

Yesu anakuja duniani jinsi iyo hiyo alienda. Haji mara mbili. Hapana mahali ambapo pametajwa katika maandiko kuunga kuja kwa siri kunyakua kanisa kulibeba na kisha kuja na watakatifu kuleta hukumu.

Kushuka kwa Bwana kutoka mbinguni kutatangazwa

**a)** ***“kwa sauti kuu”***
**b)** ***Sauti ya malaika mkuu, na***
**c)** ***parapanda ya Mungu”* (1 The 4:16).**

### Sauti Kuu

Katika agano la kale watu wa Mugu waliambiwa ***“mpigieni Mungu kelele kwa sauti ya shangwe”* (Zab 47:1).** Mwaliko ulikuwa ni kujieleza kwa sifa zenye nguvu.

Katika kuuchukua Yeriko mwaliko na tarumbeta na ***“sauti kuu*”** zilitumika katika kuziangusha kuta **(Yoshua 6:20).**

***“Mungu amepaa kwa kelele za shangwe, Bwana kwa sauti ya baragumu”* Zaburi 47:5.**

Wengine wanasema kwamba hii ni kutajwa kwa kinabii kwa kupaa kwa Yesu katika **Mdo 1:9-11**. Hakika inazungumzia sauti ya Mungu! Mtu anaweza tu kushangaa kwa nguvu na mamlaka wa mwaliko huo.

Na pia Mungu amerejesha **sauti kuu** huo miongoni mwa watu wake siku za hivi punde. Kuna sauti kuu katikati mwa watakatifu; inawezeshwa na Roho Mtakatifu; sio mwaliko wa kawaida lakini ni kutangazwa kwa Roho Mtakatifu, ikimpa Mungu utukufu na sifa!

### Sauti ya malaika mkuu

***“Sauti ya malaika mkuu”*** ni uhakika usiojulikana. Katika Biblia ni Mikaeli tu anaiitwa malaika mkuu (**Yuda 9**). Mikaeli pia anajulikana kama ***“jemedari”* (Dan 10:21)** na ***“jemedari mkuu”* (Dan 12:1).** Mikaeli alikuja kumsaidia yule aliyekuwa akiongea na Danieli (**Dan 10:13**). Hii kutajwa katika **Danieli** iko katika mazingira ya vita vya kiroho katika mbingu kati ya viumbe vya Mungu za kimalaika na utawala na nguvu za shatani.

Kwa hivyo sauti ya malaika mkuu inaweza kueleweka kuwa sauti ya Mikaeli! Mikaeli kama malaika mkuu ana mamlaka mingi na nguvu.

Kuna kutajwa mbali mbali kwa malaika katika ***ufunuo,*** kwa mfano:

- ***"Yule malaika niliyemwona, akasimama juu ya bahari na juu ya nchi…"*** **10:5**
- ***"Kisha nikaona malaika mmoja amesimama katika jua; akalia kwa sauti kuu"*** **19:17.**

Hatujui katika ujuzi wa wakati huu hali ya ukuu wa malaika wa Mungu lakini tunaweza anza kufikiria **sauti ya malaika mkuu.**

### Tarumbeta ya Mungu

***"Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadilika – dakika moja [***Kiyunani *'atomos'* ambapo tunapata neno *atom;* huu mda moja ni kama wa *atomic],* ***kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho, maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika*" (1 Kor 15:51-52)**

Siri hii inatuambia ya kwamba kuna wale **watakaosalia hai** na watakaobadilishwa mara moja Yesu atakaporudi.

***"Na hapo sauti ya baragumu ililia kwa sauti"*** Yesu aliposhuka kwa mlima Horebu kukutana na Musa na kuzungumza naye uso kwa uso (**Kut 19:19).**

Kuna mahali pengine pa kuangalia 'Baragumu' katika **Mt 24:31,** inayotuambia kwamba ***"Malaika zake [wajumbe] pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watakusanya wateule wote kutoka pepo nne"*** Pamoja "***Sauti ya baragumu".*** Baragumu hii inazungumzia kutangaza kwa injili, kuwaita watu wa Mungu, waliochaguliwa, wakusanyike.

Baragumu ilitumika kwa sababu hii kwenye jangwa na katika taifa ya Israeli.

### Baragumu

Miaka ya hivi karibuni baragumu ya kibiblia [inayotamkwa *shoh-fahr* SC#7782-Baragumu iliyotengenezwa kutoka kwa pembe za mnyama zilizopinda] imepatianwa katika kanisa kujulisha tarumbeta.

Tarumbeta ilisikika mlima Sinai, ikitangaza kushuka kwa Bwana (**Kut 19:16, 19-20).** Huu ni mfano maana baragumu itasikika tena wakati Bwana atashuka kutoka mbinguni.

Tarumbeta Ilipulizwa katika **Yoshua 6:1-20** kama silaha iliyofaa wakati wa kuanguka kwa kuta za Yeriko.

Tarumbeta ilitumika kutoa onyo (**Eze 33:2-9**) .

Tarumbeta ilitangaza siku ya upatanisho, mwaka wa jubilee (**Lawi 25:9**) na kurudishwa kwa sanduku (**2 Sam 6:15**).

### Dakika ya atomiki

Maandiko yanasema kushuka kwa Yesu kutoka Mbinguni kutatangazwa na **mwaliko, sauti** na **tarumbeta.** Hatuwezi kufikiria maajabu ya wakati huu wa 'atomiki' Wakati Bwana atashuka kutoka mbinguni akiambatana na roho za waliokufa ndani ya kristo na pengine na malaika wengi. Henoko alitabiri ***"Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu"*** **Yuda 14.**

# UHAKIKA WA KUNYAKULIWA?
## SEHEMU YA NNE

## KUKUTANA NA BWANA HEWANI

***“Nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza”* 1The 4:16.**

***“Na Roho za watu wenye haki waliokamilika”* (Ebr 12:23)** ni watakatifu ambao tayari wako mbinguni, lakini wanarudi duniani na Yesu kuipokea miili yao ya ufufuo (yenye utukufu). Katika njia ambazo haziwezi elezeka miili yao itafufuliwa kutoka duniani!

***“Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, [***watakatifu watakao kuwa duniani wakati wa kuja kwake] ***tutanyakuliwa pamoja nao [***waliokufa katika Kristo] ***katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani”* aya 17.** Huu ndio wakati ambao ***“uharibikao uvae kutoharibika, nao huu wakufa uvae kutokufa”* 1Kor 15:53.**

### Yesu anashuka kutoka mbinguni MARA MOJA

Kuna kuja mara moja ya Bwana Yesu Kristo kutoka mbinguni hata duniani: **Atashuka!** Yesu anakuja katika himaya ya dunia.

Tutamlaki ***“hewani”;***

- **Wakati** tutakaponyakuliwa kukutana naye, itakuwa hewani
- **Mahali** tutakaponyakuliwa kukutana naye, itakuwa hewani.
- Hewani ni **nini**? Ni mazingira/hali ya anga ambayo inazunguka dunia!

Neno la kiyunani linalotumika la *hewa* ni ‘aer’ na inamaanisha: hewa, ambayo inazunguka ulimwengu wote. Tunapumua hewa. Neno linaonyesha hali ya anga na hiyo ndiyo njia pekee ambayo inatumika katika Agano Jipya. Tunamlaki Yesu wapi? Hewani!

Yesu anakuja, sio kulichukua kanisa lakini kuwa na watu Wake, kanisa, duniani. Ni vigumu kuelewa vile dunia itakuwa wakati Yesu atakuja, lakini jambo moja ni hakika: tusiweke mawazo yetu ya dunia katika hatima hiyo yenye utukufu.

### Mawinguni

Hakika tutanyakuliwa ***“katika mawingu”. ‘***Mawingu’ inamaanisha nini?

**Ebr 12:1** inazungumza kuhusu watu wa imani kutoka Agano la kale walio na Yesu mbinguni kama ***“wingu kubwa la mashahidi”.*** Tunaweza kuwaza kwamba watakatifu wa Agano Jipya sasa ni sehemu ya wingu kubwa la mashahidi pia.

Pengine ‘mawingu ya nguvu’ ambayo Yesu atakuja kwayo kama alivyotabiri **Danieli** na Yesu mwenyewe katika injili hakika “***watakatifu wake, maelfu maelfu” Yuda 14.***

Katika Agano la Kale Mungu mara kwa mara alikuja katika mawingu, (**Kutoka 19:16-17; kutoka 40:34-38; 1Wafalme 8:10-11).** Mawingu yanawakilisha utukufu wa ajabu na uwepo wa Mungu, hata kama ilivyofanyika katika mlima wakubadilishwa (**Mt 17:2-5**). Mungu alijidhihirisha duniani katika mawingu na wale aliokuwa akikutana nao, walikutana na Mungu mawinguni!

Hakuna uhakika katika **1 The 4** na aya zakulinganisha ambazo tumepeana, kwamba Yesu anakuja mara mbili duniani, kwanza kuipeleka kanisa mahali na kisha baadaye kuja duniani kuhukumu wasio na Mungu.

### Na tutakuwa na Bwana milele

Mtume kisha anasema ***"na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele"* 1The 4:17.** Tutaingia kwenye wingu la utukufu wake na kila kitu kitakuwa tofauti kutoka wakati huo.

Ufahamu wowote tulio nao wa kuja kwa Bwana, jambo la muhimu ni kuwa tayari kunyakuliwa kumlaki hewani ili tuwe pamoja na Bwana milele katika utukufu wake.

## KUJA KATIKA HUKUMU

Kuja kwa Bwana kwanza kunadhihirika kwa watakatifu duniani. Wafu katika Kristo wanakuja na Yesu kutoka mbinguni, wakitumwa na Mungu, na miili yao ya utukufu itafufuliwa kutoka dunia na tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu kumlaki Bwana hewani.

Wengi wanafundisha kwamba kanisa, ambalo limefanywa na watakatifu katika kuja kwake na wafu katika Kristo ambao watakuja naye, watachukuliwa katika mbingu kwa kipindi fulani. Hata hivyo fundisho kama hilo halifai maandiko yalio wazi yalionakiliwa.

Maandiko yako wazi: Yesu **anakuja**; sio kuja na kurejea hewani na kurudi mbinguni! Haya hayafundishwi katika maandiko.

### Na watakatifu wake

Tulitaja unabii wa Henoko katika **Yuda 14** ikizungumzia wafu katika Kristo wakiambatana na Yesu kutoka mbinguni. Hata hivyo wakati tunatazama unabii huu katika mazingira ya kitengo hiki, Bwana yuaja na watakatifu wake ***"Ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu yake"* Yuda 15.**

### Kufanya hukumu

Watakatifu wanakuja na Yesu kufanya hukumu. Hawaendi mbinguni kwa likizo ya mda wakati shetani anatawala duniani kupitia mpinga-Kristo akileta uoga.

Watakatifu wanahusisha wafu katika Kristo ambao wamepokea miili yao ya ufufuo na watakatifu ambao wako uhai duniani, ambao watainuka kumlaki Bwana hewani pia wakiipokea miili yao yenye utukufu.

Yesu Kristo yuaja na hukumu katika dunia. Watakatifu wake walio kweli, wanaoamini na waliotakaswa ambao wamekwisha tukuzwa ndani yake na kuunganishwa na yeye hewani, watakuja na yeye kutawala na kutamalaki na yeye duniani kwa 'miaka elfu moja' [miaka elfu ni kipindi kisicho elezeka].

Hukumu itatendeka ***"katika siku hiyo"*** wakati Yesu atakapo kuja ***"ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustajaabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile"* 2 The 1:10.**

### Ni lini wasioamini na wasiotii watahukumiwa?

***"Yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile"* 2The 1:10.**

### Kuja kwa Bwana kunaleta mambo mawili ya muhimu

1. Kutukuzwa kwa watakatifu.
2. Hukumu ya waasi.

### Mambo haya yanatendeka lini?

- Kuja kwake kwa hukumu ni siku moja na wakati atakapotukuzwa katika watakatifu wake.
- Atatukuzwa katika watakatifu wake wakati watapokea miili yao ya utukufu.
- Haya yatatendeka wakati ***"tutamuona kama alivyo, atakapodhihirishwa, tutafanana naye"*** **(1Yn 3:2);**
- Wakati ***"tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani"*** **(1The 4:17).**

### Ni wakati wa kufikiria tena ufahamu wetu wa kuja kwa Bwana

Katika msururu wa sehemu hizi nne zinazoshugulikia uhakika wa kunyakuliwa, tumetafuta kwa kutamatisha kutoka kwa kuyaleta maandiko wazi, bila kuongeza wala kupunguza, kwamba kunyakuliwa ni mafundisho ya mwanadamu yalioingia katika mafikira ya mkristo na mahubiri kutoka mwaka wa 1820. Fundisho hili lilianza na 'ufunuo' wa binafsi ambao haukutokana na maandiko katika maneno ya kinabii. Kila unabii ni lazima uhukumiwe na upimwe kulingana na maandiko (**1The 5:20-21**).

Fundisho la kunyakuliwa limeinuka juu ya fundisho la muhimu la biblia la kufufuliwa wafu na limelifanya kanisa kuwa dhaifu kuweza kusimama kinyume cha mawimbi ya mpinga Kristo ambayo kwa wakati huu yanafagia dunia. Badala ya kuwatia nguvu waamini wasimame na wakemee roho ya mpinga Kristo, wakristo wanangojea kuchukuliwa kisirisiri kwa haraka wapelekwe mbinguni ili wajiepushe na adha na dhiki. Hii ni tumaini lisilo la kweli na kanisa ni lazima lifanywe wanafunzi na wafundishwe neno la Mungu kwa njia ile ile mitume wa kwanza walitufundisha.

### Kutakuwa na waalimu wa uongo

Petro anatuonya ***"hakuna unabii katika maandiko upatao kutafsiriwa kama apendavyo mtu fulani tu"*** **(2 Pet 1:20).** Anaendelea kutuonya:

> ***"Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutavyokuwako <u>waalimu wa uongo</u>, watakaoingiza kwa welevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia".***
> [fundisho la kunyakuliwa ni kupotoka kwa uharibifu na inanyima watu ushindi wa Yesu Kristo kupitia kufa kwake na kufufuka kwake.]
>
> ***"Na wengi watafuata ushahidi wao; na kwa hao njia ya kweli itatukanwa.***
> ***Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliotungwa; ambao hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii"*** **2Pet 2:1-3.**

# KAMA ILIVYOKUWA SIKU ZA NUHU

*"Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake. Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwa mwana wa Adamu. Wakati ule watu wawili watakuako kondeni; mmoja atwaliwa, mmoja ataachwa; wanawake wawili watakuwa wakisaga; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa. Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. Lakini fahamuni neno hili; kama mwenye nyumba analijua ile zamu mwivi atakayokuja, angalikesha, wala asingaliiacha nyumba yake kuvunjwa. Kwa sababu hiyo ninyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja"* **Mt 24:36-44**. [tafadhali soma **Lk 17:26-36]**

## KATIKA SIKU ZA NUHU

***"Maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani; … kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote"* Mwa 6:5**
***"BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani"* 6a**
Akasema, ***"nitamfutulia bali mwanadamu … usoni pa nchi"* 7a**
***"Lakini Nuhu akapata neema machoni pa BWANA"* aya 8**

***"Mungu akamwambia Nuhu, 'mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia'"* aya 13**
***"Na tazama, nitaleta gharika ya maji juu ya nchi, niharibu kila kitu chenye mwili na pumzi ya uhai"* aya 17a**
***"Lakini nitafanya agano langu nawe kuwa dhabiti"* aya 18a**
***"Ndivyo alivyofanya Nuhu, sawasawa na vyote alivyomwamuru, hivyo ndivyo alivyofanya"* aya 22**

### Kulikuwa na uasi mwingi, uovu na uhalibifu

Katika siku za Nuhu kulikuwa na maasi mengi duniani; mioyo ya wanadamu ilipatianwa kwa maovu, dunia ilijaa uharibifu. Hii ilikuwa ni ya kusubua na kuvunja moyo kwa Mungu kwa maana alikuwa amemuumba mwanadamu kwanza kwa mfamo wake na sura na alikuwa na mpango mzuri kwa mawazo yake kwa watu wote. Lakini watu wa dunia waligeuka kinyume cha Mungu na watu wengi waliishi kwa sababu yao, bila uzuri na uungu wa kweli.

### Paulo alitabiri wakati kama huo

Paulo alieleza wakati kama huo ukija duniani tena. Akasema, **"*Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazzi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka***

***kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake"*** **2 Tim 3:1-5.** Tunaishi nyakati hizo?!

### Mungu alimpata mtu mmoja

Mungu alikusudia kuhukumu dunia na uasi wote ndani yake. Akampata mtu mmoja, Nuhu, ambaye alikuwa akitembea katika neema, akimuamini Mungu na akiwa anatamani kumtii Mungu. Twaijua hadidthi: ni jamii ya karibu ya Nuhu ambayo ilikuja kwa imani hiyo ya kuokoa kama Nuhu. Mungu aliahidi kuyafanya maagano na Nuhu na kumuokoa kutoka hukumu ya gharika, alimhifadhi Nuhu na jamii yake kutoka uharibifu, kwa kuwa walikuwa katika maagano na Mungu.

### Mungu alimhifadhi Nuhu

Mungu alimhifadhi Nuhu na jamii yake na ndege wawili wawili wa kila aina na wanyama duniani, ili wawezi kuirithi dunia. Mungu akarudia kwa Nuhu kusudi lake la uumbaji kwa Adamu na Hawa, ***"Mungu akambariki Nuhu na wanawe, akawaambia, zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi"*** **Mwa 9:1.** Mathumuni ya Mungu ilikuwa awe na watu wa agano duniani ambao watakuwa wenye haki, wakitembea katika neema yake. Ahadi ilikuwa ni kwa Nuhu na uzao wake (**aya 9**).

> ***"Bwana akamwambia Nuhu, 'Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki'"*** **Mwa 7:1.**
> ***"Ikawa baada ya siku hizo saba, maji ya gharika yakawa juu ya nchi"*** **aya 10**
> ***"Wakafa wote wenye mwili waendao juu ya nchi: ndege …, na kila mwanadamu"*** **aya 21**
> ***"Akabaki Nuhu tu, na hao walio pamoja naye katika safina"*** **aya 23b**
> ***"Na Mungu akamkumbuka Nuhu, na kila kilicho hai, na wanyama wote waliokuwamo pamoja naye katika safina"*** **Mwa 8:1.**

## KUJA KWA YESU

### Kuja kwa Yesu: wakati wa hukumu

Yesu alisema kwamba masharti ambayo watakuwapo wakati wa kuja kwake itakuwa ***"Kama ilivyokuwa siku za Nuhu".*** Hii inaonyesha kwamba umati mkumwa wa wanadamu watakuwa wamejipatiana kwa Mungu, kuzitafuta njia zake na kuishi kulingana na mpango wake. Inaonyesha wazi pia wakati wa hukumu baya ikija duniani ambayo itauharibu uovu, mawazo mabaya na uharibifu utakaokuwapo duniani. ***"Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya BWANA, dunia na wote wakaao ndani yake"*** **Zab 24:1.**

### Waasi wataangamizwa

Mungu hakuiumba dunia kwa sababu ya waasi; pia hakuiumba kuzimu kwa wanadamu. Aliumba kusimu kwa shetani na malaika walioanguka, lakini wale ambao wanasisitiza kupinga BWANA wakiwatesa watu wake, wataiona hukumu katika ***"moto wa milele"*** **Mt 25:41.**

Paulo anadhibitisha haya katika **2The 1:7b – 10a**, ***"wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbiguni pamoja na malaika wa uweza wake; katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake; yeye atakapokuja".***

### Maisha ya kila siku yanaendelea mpaka…

Yesu alisema kwamba hatujui saa, lakini alitupa maagizo ili tufahamu itakuwa namna gani. Maisha yalikuwa ya kawaida siku za Nuhu, mpaka siku ile Nuhu aliingia safina. Gharika ikaja na ikawaondoa wote mbali. Kama siku za kuja kwa Mwana wa Adamu ni kama siku za Nuhu, basi kuna matarajio ya hukumu ya dunia yote ambayo mwisho itatenga waovu kutoka kwa wenye haki.

### Ni nani aliondolewa?

Hili ni swali la muhimu sana. Tunajua wazi kutoka kitabu cha **mwanzo** ya kwamba waovu waliondolewa na gharika. Gharika ilikuwa yenye uharibifu mkubwa sana, ikivunika dunia yote, ikiharibu hata milima mirefu. Gharika iliwaondoa waasi ulimwenguni – hawakuwepo tena!

### Walichukuliwa na nini?

Walichukuliwa na gharika. Gharika ndio ilikuwa hukumu ya Mungu juu ya maasi yaliyokuwemo duniani kwa sababu ya tabia za mwanadamu, mawazo na matendo. Waasi duniani waliondolewa kwa hukumu. Hawakubaki duniani na hakika hawakupelekwa mbinguni. [Tafadhali soma **1 Pet 3:18-20**].

### Ni nani aliyebaki siku za Nuhu?

Ni Nuhu peke yake na jamii yake walibaki duniani. Tambua **<u>walibaki duniani!</u>**

Walijithibiti hukumu! Kwa hakika walihifadhiwa na neema ya Mungu katika safina ya wokovu iliyopatianwa na Mungu.

Hawakutolewa nje ya, ama kutoka ulimwenguni. Walihifadhiwa duniani na dunia ikawa urithi wao, waliopewa na Mungu baada ya hukumu kutakasa maovu yote duniani.

### Dunia yenyewe haikuharibiwa

Mungu alisema ***“nitawaharibu [***waasi] ***pamoja na dunia”*** **mwa 6:13.** Lakini Mungu hakuiharibu dunia haswa. Mungu hatawahi haribu dunia kwa maana ni kiumbe chake. [ona **mhubiri 1;4, zab 104:5, zab 119:90**].

Wakati Mungu alimaliza kuumba dunia na kila kitu kilicho duniani, alisema ***“na tazama ni chema sana”*** **(mwa 1:31).** Sio dunia iliyoumbwa ambayo inamkasirisha Mungu lakini ni tabia za mwanadamu ambao hawajiharibu tu na wengine, lakini pia wanaharibu dunia. Wazee 24 walisema kwamba Mungu anapaswa ***“kuwaharibu wao waharibuo nchi”*** **ufu 11:18.**

### Wenye haki watarithi dunia

Dunia haitapatianwa kwa waasi, lakini wenye haki watarithi dunia. ***“Mwenye haki hataondolewa milele; bali wasio haki hawatakaa katika nchi”*** **mithali 10:30.**

Kwa sababu yoyote, waamini wengi hawafurahii dunia katika kusudi la Mungu kuiumba na tumefundishwa ya kwamba tumeokolewa twende mbinguni. Mafundisho kama hayo hakika sio maandiko. Tumeumbwa tukamilishwe na kurejeshwa katika sura na mfano wa Mungu. Tumeokolewa katika ufalme wake, ***“ufalme wa mwana wa pendo lake”*** **(Kol 1:13).**

### Viumbe vitarejeshwa

Tumeokolewa tulete urejesho duniani: ***“kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu. … kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa***

***utukufu wa watoto wa Mungu”*** **Rum 8:19, 21.** Uhuru haujafunuliwa bado katika maisha ya watoto wa Mungu duniani, lakini andiko hili liko wazi: watoto wa Mungu watafurahia uhuru wa utukufu duniani; zaidi sana, ya kwamba viumbe vyote vitaletwa kwenye uhuru na utukufu wa Mungu utatandaa kwa kila kitu.

### WAWILI WATAKUWA KONDENI

Katika mazingira ya kutuambia kuja kwake kutakuwa kama ilivyokuwa siku za Nuhu, Yesu akaongea kuhusu watu wakiendesha maisha yao kama kawaida: wengine wakifanya kazi kondeni; wengine wakisaga; wengine wakilala usiku. Kisha akasema katika kila hali kwamba ***“mmoja atwaliwa, mmoja aachwe”*** [soma maandiko haya kwa kumakinika: **Mt 24:40-41; Lk 17:34-36].**

### Ni nani atwaliwa?

Kumbuka Yesu alisema, ***“na kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku zake mwana wa Adamu”*** **(Lk 17:26).** Nani alitwaliwa siku za Nuhu? Waasi walitwaliwa na gharika: “***Gharika ikashuka ikawaangamiza wote”*** siku ile Nuhu aliingia kwenye safina **(Lk 17:27**). Hukumu inawatwaa waasi. Waasi wanatwaliwa na hukumu: wanaangamizwa!

Kisha Yesu akasema, ***“na kadhalika, kama ilivyokuwa siku za Lutu, walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakinunua na kuuza, wakipanda na kujenga; lakini siku ile Lutu aliotoka Sodoma kulikunya moto na kiberiti kutoka mbinguni vikawaangamiza wote”*** **Lk 17:28-29.** Katika hukumu hiyo ya kutisha, Lutu na binti zake waliokolewa na wakahifadhiwa duniani; waasi walioishi sodoma walitwaliwa na hukumu; waliangamizwa.

### Ni nani ataachwa?

Ni nani aliyeachwa siku za Nuhu? Ni Nuhu tu na jamii yake walioachwa! Ni wenye haki tu walihifadhiwa siku ya hukumu. Ilikuwa vivyo hivyo siku za Lutu.

Ni nani atakayeachwa siku za mwana wa Adamu, wakati huo wa hukumu ya kutisha ***“wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake; katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu”*** **(2The 1:7b-8).** Waasi wataharibiwa, lakini wenye haki watapewa ***“raha”*** (**Aya 7a**) ***“katika siku hiyo”*** **(Aya 10).**

### Watakatifu watakuwa duniani

Watakatifu watakaokuwa duniani wakati Yesu atakapokuja, watatukuzwa ndani yake (**2 The 1:10**); waasi wataangamizwa kwa kuja kwake. Wataangamizwa ***“kwa pumzi ya kinywa chake”*** **2The2:8**. Aya hii inazungumzia yule ‘asi’, lakini pia inaweza kuzungumzia uharibifu wa waasi na wasiotii [soma kwa makini **Mt 13:41-42** kuona kwamba wasiotii wote wataondolewa duniani].

## MAFUNDISHO YA KAWAIDA YA KUNYAKULIWA

Wengi wamefundiswa kwamba ‘***anayetwaliwa’*** katika aya zilizo juu ananyakuliwa mbinguni na kwamba waasi wanaachwa watawale dunia. Haikutendeka hivyo siku za Nuhu na hayo sio hayo yalitendeka siku za Lutu. Hakuna sababu ya maandiko au ushahidi wa kusoma ‘kunyakuliwa’ katika aya hizi wakati ni maneno ya Yesu mwenyewe kuhusu kuja kwake.

Ninaelewa kuwa mafundisho haya, ambayo iko wazi/imenyooka, kunapingana na mafundisho yenye kujulikana, sio tu kwa jukwaa lakini pia katika vyuo vya Biblia. Nawaombeni kujifunza kuyasoma maandiko katika mazingira. Maandiko mengi hayahitaji utafsiri; yanahitaji tu kusomwa katika mazingira wazi na uaminifu. Kama watu watafanya haya, wakati huu na ujao itakua imehakikishwa kwetu kwa imani katika neno la Mungu, na tutarithi utimilifu wa utukufu wa Mungu duniani.

***“Lakini hakika yangu, kama niishivyo, tena kama dunia hii nzima itakavyojawa na utukufu wa BWANA”***
***Hesabu 14:21.***

# INJILI YA UTUKUFU

**na Nicholas Jackson**

Wakati nakala hii, 'Kama ilivyokuwa Siku za Nuhu', ilitolewa kama gazeti mnamo mwezi wa Tisa 2010, kulitokea changa moto na maswali kuhusu fundisho hili. Majibu yafuatayo yalifuata kama jawabu ya maswali mwezi wa kumi, 2010. Tunafahamu kwamba fundisho hili linaenda kinyume cha kawaida ya mafundisho ya kanisa la wakati huu ambayo inalenga kuleta picha ya siku za mwisho [mambo ya nyakati za mwisho] ambayo inatilia umuhimu wa jambo linaloitwa 'kunyakuliwa'. Hii imefundisha kanisa kutafuta njia ya kuepuka kuliko kusimama katika ushindi wa Masihi Yesu ulimwenguni.

### Ufunuo unaoendelea kufunguka wa neno la Mungu

Mungu anaendelea kufungua ufunuo wa neno lake kwetu tunapotembea na yeye na kila mmoja wetu. Ni wakati wetu sisi sote tulio washirika wa mwili wa Kristo kunyenyekea na kuruhusu neno la Mungu litunenee, sio kudhania kwamba tunajua linasema nini kabla ya kulisoma.

### Mungu atafunua mambo yote

Paulo anawaandikia wafilipi, na pia sisi, kwamba tunapaswa kuwa na mawazo ya ***"Kukasa mwendo, nifikilie mede ya dhawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu. Basi sisi tulio wakamilifu na tuwaze hayo; na hata mkiwaza mengine katika jambo lolote, Mungu atawafunulia hilo nalo"*** **(Flp 3:14-15).** Mungu anataka sisi sote tutembee pamoja katika **mwawazo yaliyo komaa**, hivyo ni, katika nia ya kutaka kupatiana kila kitu kwa sababu ya Yesu na injili. Wakati tunafanya, hata pale ambapo hatuyaoni mambo kwa pamoja, tunaweza kutumaini kwamba **Mungu atafunua** maeneo ambayo tuna shaka.

### Tusiende zaidi ya yaliyoandikwa

Ni ya muhimu sana kuingia katika ***"roho ya hekima na ufunuo katika kumjua yeye*** **[Yesu Kristo]*"* Efe 1:17.** Kama sivyo tunafanyika ***"wenye akili*"** **Rum 11:25** na ***"asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe"*** **(1Kor 4:6c).** Mtume Paulo anatuonya ***"kujifunza kutokupita yale yaliyoandikwa"*** **(1 Kor 4:6b).**

Hebu tujipatiane kwa ufunuo unaofunguka wa neno la Mungu, tukikubali ya kwamba hatuna maarifa na ufahamu kamili, lakini tuna maandiko ***"ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu"*** **(2Tim 3:15b).**

## MUNGU ANATUREJESHEA INJILI YA USHINDI!

Tangu kuanzishwa kwa mafundisho ya kunyakuliwa katika mapema 1800, kumekuwa na upungufu kanisani, ya kuamini katika ushindi wa injili na Umasihi wa Yesu. Yesu tayari ni Mfalme. Tayari ametukuzwa kwa enzi ya Mungu na anatawala na kutamalaki mbinguni na ulimwenguni sasa (**Mdo 2:33-36; Mt 28:18**).

Wengi wamekuwa wakitafuta kutorokea hali za dunia ambazo wanaona zikidhoroteka katika kupotoka kwa kanisa, serekali ya mpinga-kristo katika mataifa na kutotii sheria kupitia vizazi vyote. Wanangojea kunyakuliwa iwapeleke mbinguni wakiacha dunia itawaliwe na shetani.

### Kuhubiri na kufundisha Yesu kama masihi

Mitume wa kwanza walikuja wakihubiri injili nyepesi lakini yenye upana sana: ***"Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo"*** **(Mdo 5:42).** Maisha ya mwisho ya mtume Paulo ilitumika ***"akihubiri habari za ufalme wa Mungu na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi"*** **(Mdo 28:31).**

Mtume Paulo aliteseka mambo mengi kwa injili hii lakini aliweza kutangaza ***"ni nani atakaye tutenga na upendo wa Kristo? Je! ni dhiki au shida, au adha au jaa, au uchi, au hatari, au upanga? Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliye tupenda"*** **(Rum 8:35,37).**

### Ni lazima atawale

Kuhubiri Yesu kama Masihi ni kuhubiri kwamba Yesu ni Mfalme. Kuhubiri ufalme wa Mungu ni kutangaza utawala wa Mungu ulimwenguni kupitia Masihi, kwamba ***"Ni lazima atawale mpaka adui zake wote wawekwe kuwa chini ya miguu yake"*** **(1Kor 15:25).** Kupitia kuhubiri ***"hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi kwa falme na mamlaka"*** **(Efe 3:10),** maadui wake wote watamuinamia!

Tunaweza kuteseka kwa kuyahubiri haya, lakini tuna ahadi kwamba ***"kwa kuwa ni haki mbele za Mungu kuwalipa mateso wale wawatesao ninyi; na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni"*** **(2The 1:6-7).** Hata Nebukadreza ilimpasa ajifundishe kupitia uchungu wa moyo kwamba ***"mbingu ndizo zinazo tawala!"*** **(Dan 4:26b).** Hatuko katika vita vya kushindwa: mfalme wetu ameshinda na hatutapumzika mpaka ***"Atakapoufanya imara Yerusalemu, [*****picha ya kanisa aliye bibi arusi]** ***kuufanya kuwa sifa <u>duniani</u>"*** **(Isaya 62:7)**

### URITHI WETU – MBINGUNI AU DUNIA?

Ushuhuda wa maandiko ni kuwa Mungu anahifadhi na kulinda wenye haki katika hukumu ya waasi. Alimhifadhi Nuhu duniani wakati waovu walihukumiwa. Kama watu wengi wangependa kubishana kwamba Nuhu "alitwaliwa" juu ya gharika na hiyo inatuonyesha kwenda mbinguni katika wakati wa hukumu, ukweli unabaki kwamba Nuhu alibaki katika himaya ya ulimwengu. Mungu hakumwondoa katika uharibifu lakini alimlinda katikati yake.

Pia ni ya kupendeza kwamba Yesu akija, tutamlaki hewani, hivyo ni, katika himaya ya ulimwengu (**1The 4:17).**

### Ni waovu watakaoangamizwa

Wakati Yesu atakapokuja, imeandikwa kwamba ***"watakaoadhibiwa [*****wasio na Mungu na wasio tii]** ***kwa maangamizi ya milele … yeye atakapokuja, katika siku ile kutukuzwa katika watakatifu wake"*** **(2 The 1:9-10a).** Elewa kwamba mambo mawili yalitendeka kwa wakati mmoja na hakuna aliyeenda pahali. Uharibifu wa waasi ulifanyika wakati mmoja watakatifu wanapotukuzwa na yule mtu ambaye ametoka pahali pamoja hadi kwingine ni Bwana Yesu peke yake kwa kuwa ***"umefunuliwa kutoka mbinguni"*** katika himaya ya dunia. **1 The 4:16** anasema, ***"kwa sababu Bwana mwenyewe <u>atashuka</u> kutoka mbinguni".***

### Dunia kweli itaharibiwa?

Mungu alisema katika siku za Nuhu ***"Basi nitawaharibu [waasi] pamoja na dunia"*** **(Mwanzo 6:13b);** dunia haswa haikuharibiwa.

Petro anasema, ***"kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji"*** **(2 Pet 3:6).**

Ulikuwa ni uasi wa duniani na mipangilio miovu ambayo iliharibiwa: ni njia ya maisha ambayo iliharibika.

Nuhu, aliilithi dunia mpya – mahali ambapo uovu ulikuwa umeondolewa na ambapo Nuhu, ambaye alikuwa ***"mwenye haki mbele zangu [Mungu] katika kizazi hiki"*** **(Mwa 7:1),** angedumu na amani.

Hivyo hivyo Petro anasema ***"lakini, kama ilivyo ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake"*** **2 Pet 3:13.** Tambua kwamba mbingu mpya na dunia mpya zinaonekana kuwa ni pahali ambapo haki inadumu, hivyo ni, ambapo watu wanatembea kwa imani katika Yesu Kristo wakipokea neema yake.

Yesu alisema kwamba ***"Yesu alisema kwamba wapole watairithi nchi"*** **(Mt 5:5)** na pia akatufundisha kuomba ***"ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe <u>hapa duniani</u> kama huko mbinguni"*** [**Mt 6:10].**

**Mpango wa Mungu ni kwamba dunia ipate kumilikiwa na watu wanyenyekevu ambao watapokea utawala wake wa kifalme na kuomba waone uhakika wa maisha ya mbinguni hapa duniani.**

## Ufalme wa mbinguni unafunuliwa hapa duniani.

Mfano wa ngano na magugu katika **Mathayo 13** ni mfano kuhusu ufalme wa mbibguni. Wakati Yesu alitafsiri mfano huo alisema kwamba ***"lile konde ni ulimwengu"*** **Mt 13:38.** Yesu anasema ufalme wa mbinguni uko wapi? Uko duniani! Ufalme wa mbinguni unatakiwa uonekane duniani na tumezaliwa upya tuingie ndani **(Yn 3:5-6**).

## Wana wamepandwa duniani

Anawapanda wana wa ufalme duniani na wanakua pamoja na magugu ambao ni wana wa yule mwovu. Wakati wote wamekomaa, wakati wa mavuno unakuja ambapo **"*Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake/ wajumbe, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake [*****ambao uko katika ulimwengu] ***machukizo yote, na hao watendao maasi na kuwatupa katika tanuru la moto"*** **Mt 13:41-42a.**

***"Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao"*** **Mt 13:43.** Ufalme wa mbinguni unafunuliwa duniani bila maovu; moto umewachoma wote (**2Pet 3:10-12**).

## VIPENGELE VITAYEYUKA VITAUNGUZWA NA KUFUMULIWA

Ni ya kupendeza kuona kwamba neno neno lililotumika kwa vipengele katika **2 Pet 3:10, 12** ni jina moja na lile limetumika katika **Kol 2:8**, na limetafsiriwa, ***"mafundisho ya awali";*** katika **Kol 2:20,** pia tena ***"mafundisho ya awali".*** Katika **Gal 4:3, NKJV** inatafsiri 'vipengele': ***"tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia".***

Neno hilo hilo linatumika katika **Gal 4:9 "*kwa nini kuyarejea tena mafundisho ya kwanza yaliyo manyonge yenye upungufu, ambayo mnataka kuyatumikia tena".*** Pia inatumika katika **Ebr 5:12** kwa mazingira ya njia nzuri na inatafsiriwa kama **mafundisho ya kwanza, *"mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu".***

*Vipengele* vinatafsiri neno la Kiyunani "*stoicheion"* na inaonekana katika Strong's Concordance Gr #4747. Neno hili linamaanisha: kitu ambacho kimewekwa kwa mpangilio katika kupangwa. Kimsingi inamaanisha 'Kuwa sehemu/au sehemu ya yote' na kwa njia ya kulinganisha na mambo ya kweli. Inaweza kutumika kwa njia nzuri au baya, na katika Biblia

inatumika sana kwa njia iliyo kinyume ya kanuni isio na umuhimu mkubwa ya dunia hii ambayo tunapaswa kukombolewa kwayo na neema ya injili. Tunapaswa kuishi na mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu.

Katika mazingira haya hakika neno linatumika kueleza mafundisho ya msingi ya elimu ya ulimwengu. Ni mafundisho ya dunia, mafundisho ya uongo na mafundisho ya mapepo ambayo yanaleta utumwa kuliko uhuru, ambayo inapatikana katika ukweli wa neno la Mungu (**Yn 8:32**)

### Neno ni kama moto

Mungu alisema kupitia Yeremia, ***"je! neno langu sio kama moto"*** **(Yer 23:29).** Ni moto wa neno la Mungu ambalo linachoma viumbe dhaifu, mafundisho ya uongo ya dunia, ili haki ibaki tu: mbingu mpya na nchi mpya.

Yesu alisema, ***"Nimekuja kutupa moto duniani; na ukiwa umekwisha washwa, ni nini nitakalo zaidi"*** **(Lk 12:49).** Alikuwa akizungumza kuhusu kuhukumu yule mtumwa ambaye alitumia mamlaka yake vibaya (**Lk 12:42-48**) na alikuwa karibu kuanza kushiriki vile hakuja kuleta amani, lakini upanga na hata kuzitenganisha jamii za asili (**aya 51-53**). Alikuja kuleta hukumu! Moto wa neno lake ndio alileta duniani!

### Kuimarisha ufalme; siri kufunuliwa

Mungu yuko kazini akiimarisha ufalme wake duniani. Danieli alisema kwamba itakuwa kama ***"Na lile jiwe…likawa mlima mkubwa, likajaza dunia yote"*** **(Danieli 2:35).** Kisha akasema kwamba ufalme huu "***utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu"*** **(Danieli 2:44).** Ufalme huu hata hivyo ***"naye atamiliki hata milele na milele"*** [ona **ufu 11:15**].

Injili ambayo Yesu na mitume walihubiri, ilikuwa ni injili iliyofunua utukufu na nguvu za Yesu aliye Masihi, mfalme, ambaye ni mtawala ***"Mkuu wa wafalme wa dunia"*** **(Ufu 1:5).**

Ni injili ambayo itatamalaki kwa ushindi katika kila kizazi mpaka utukufu wake ufunuliwe duniani – utukufu ambao unaonekana katika uso wa Yesu Kristo (**2 Kor 4:6**) kama "***akalifunua neno lake kwa majira yake katika ule ujumbe"*** **(Tito 1:3)**

Siri ni katika Kristo, Mungu anavileta vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani pamoja ndani yake (**Efe 1:10**).

**Mbingu zitaonekana zikitawala duniani!**

## NI NANI ALITWALIWA?

Baadhi ya watu wanaonekana kuwa na uhakika kwamba katika **Mt 24:39** Yesu alikuwa akiongea habari za Nuhu na Jamii yake kuchukuliwa na gharika. Tafadhali soma tena kifungo hiki kwa makini na kwa kuaminika.

Katika **aya 39** inasema ya kwamba ***"wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukuwa wote".*** Nuhu na jamii yake walijua Gharika inakuja; ndiposa Nuhu akaijenga safina!

Ni kweli kwamba Yesu alisema Mwana wa Adamu atakuja kwa saa ambayo hatutarajii. Hata hivyo, Paulo anasema katika **1The 5:2-5, "*Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, kuna amani na salama,***

***ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula … <u>wala hakika hawataokolewa.</u> Bali ninyi <u>ndugu, hammo gizani</u>, hata siku ile iwapate kama mwivi, kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana, <u>sisi si wa usiku, wala wa giza,</u>"***

Paulo anasema kwamba kama tuko katika nuru, tutakuwa tayari kwa siku na haitatuchukua, ama iwe ya ghafla na isio tarajiwa.

Waasi duniani katika siku za Nuhu **hawakujua mpaka gharika ikaja na kuwachukua.** Nuhu alijua kikamilifu yaliyokuwa yakitendeka – alikuwa amejiandaa kwa ajili yake kwa muda. Alikuwa mwana wa mchana!

# MANENO MUHIMU KATIKA MATHAYO 24:39-41

**Mathayo 24:39** **"*Gharika ikaja, ikawachukua wote*"**

**Kuchukua** SC# 142 Gr. *airo,* neno la msingi, *kuinua*;
Kwa kuelewa, *kuondoa* au *kuchukua juu.*
Kwa kulinganisha inaweza kumaanisha *kuinua sauti;* pia *kusafirisha;*
Katika mazingira ya Kiebrania, inamaanisha *kuondoa dhambi.*

- **Imetafsiriwa katika KJV:-** kuinua juu[32x], kuondoa [25x], kuchukua [25x], bali na [5x], inua juu [4x], kuchukua [3x], na mengine 8.

**Mathayo 24:40** **"*wawili watakuwako kondeni, mmoja atwaliwa*"**

**Kutwaliwa** SC# 3880 Gr. *Paralambano*
Kutoka # 3844 *para,* karibu, kutoka kando, katika pahali unaonekana.
#2982 *lambano*, kuchukua [katika maeneo kwingi], imetafsilrwa: pokea *[*133x*]*, chukua *[*106x].
*#3880* ikimaanisha: *kupokea karibu,* kwa mfano, *kushirikiana na wewe binafsi; kupokea ofisi; (*kulinganisha) *kusoma.*

- **Imetafsiriwa katika KJV:-** chukua [30x], pokea [15x], chukua hadi [2x], kuchukua juu [2x], kuondoa [1x].

"Vines Expository Dictionary" inapatiana maana sawa: *kupokea au kujiletea au niwe nayo.*

Vines*'* inaongea juu ya **Mathayo 24:40 – "***kuhusu kuondoa watu kutoka dunia katika hukumu, wakati Mwana wa Adamu atafunuliwa".*

Vines' Inaongea kuhusu **Luka 17:34-35** na neno lile lile 'kutwaliwa' – "*maana ya kuondolea kutoka uharibifu".*

Neno *kutwaliwa* linatumika katika **Mathayo 27:27** wakati Yesu alichukuliwa na askari kwa sababu ya kuchapwa viboko; na katika **Yohana 19:16,** Yesu anachukuliwa akasulibiwe.

**Mathayo 24:40-41** **"*Mmoja atwaliwa, mmoja aachwa*"**

**Aachwa** SC# 863 Gr. *aphiemi,* kutuma, katika maeneo kwingi [ikihushisha kufuata]

- **Imetafsiriwa katika KJV:** acha [52x], samehe [47x], teseka [14x], ruhusu [8], kuachwa [6x], acha peke yake [6x], na mengine 13.

Vines Expository Dictinary, inapatiana maana kama: *kufukuza* au *kutuma.*

**Amen!**